Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 78 No. 197 | DH. QAD-DH. HIJ. 1439 AH | SEPTEMBA 2018 | IKHA 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimari-shia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. ***(An-Nuur 24:56).***

Jalsa Salana Uingereza 2018 Yafana

Na Mwandishi Wetu



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 10/08/2018, baada ya Tashahhud, Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Alhamdulillah, Jalsa Salana ya Uingereza ilimalizika Jumapili iliyopita kwa kueneza baraka zake na fadhili za Allah chungu nzima. Siku hizi tatu zilikuwa zenye baraka mno.

Maandalizi ya Jalsa Salana yanaendelea mwaka mzima lakini katika miezi mitatu au minne ya mwisho hususan uongozi na wengi wa wanaojitolea wanaanza kushughulika katika maandalizi. Katika wiki mbili za kabla ya Jalsa Salana idadi ya wafanyakazi wanaojitolea pia huongezeka.

Hususan kwa ajili ya kuleta faraja za kila aina katika Hadiqatul Mahdi, hawa wanaojitolea hufanya kazi kwa kutumia uwezo wao wote. Wengi wa wanaojitolea ni Khuddam. Kazi ya kuibadilisha sehemu iliyoonekana kama pori kuwa mji kwa muda mfupi si kazi rahisi. Cha zaidi ni wanaojitolea si wale ambao wana ujuzi wa utaalamu wa kufanya kazi hizi zote. Lakini yote yanayotokea ni kwa mujibu wa fadhili za Allah. Allah ndiye anayestawisha juhudi hizi zote kwa mafanikio makubwa. Na wageni wanaokuja pia hushangaa kwa kuona shauku ya vijana wanaojitolea.

Kabla ya Jalsa Salana wafanyakazi huendelea na kazi zao lakini katika siku za Jalsa, idadi yao huongezeka na vijana wengine, wazee, kinamama na watoto wote hushiriki katika huduma hizo. Hili ni jambo la ajabu kwa wale wageni wasio Waahmadiyya kwamba namna gani watoto na wazee wote wanavyojitolea na kufanya shughuli zao.

Wageni ambao hawana uzoefu wa kazi hii huwa wanavutiwa sana na kazi ya hawa wanaojitolea. Na jinsi wageni wanavyoeleza maoni yao, bila shaka ni maelezo ya kipekee. Pamoja na kusifu huduma za wanaojitolea wageni hueleza katika maoni yao kwamba Jalsa imeacha athari nzuri na kubadilisha maisha yao. Pamoja na kuwa sio Waislamu lakini athari nzuri ya mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam imepatikana katika maisha yao, wamepata maelezo zaidi kuhusu Islam na kuhusu Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya na badala ya kupata athari isiyofaa wameweza kujua uzuri wa mafundisho ya Islam.

Basi upande mmoja kama Jalsa salana huimarisha imani ya Wanajumuiya na kuongeza udugu kati yao, upande wa pili

Endelea uk 4

Tanzania Yaiwakilisha Afrika Ba'iat ya Kimataifa

Na Mwandishi Wetu

Kwa msaada mkubwa wa Allah Tanzania imepata heshima kubwa kwa uteuzi wa Sheikh Bakri Kaluta Amri Abedi ambaye ni Naibu Amiri wa Tarbiyyat na Tabligh kuteuliwa kuiwakilisha Afrika katika Baiat ya kimataifa iliyofanyika katika mkutano wa mwaka wa 2018 jijini London nchini Uingereza.

Mkutano huo wa 52 wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ujulikanao kama ***Jalsa Salana*** ambao una taswira ya kimataifa kwa sababu ya kuhudhuriwa na kiongozi mkuu wa kiroho wa Jumuiya ulihudhuriwa na watu pamoja na wawakilishi 38,000 kutoka nchi 118 duniani.

Jalsa Salana ambayo ilianzishwa na mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. mnamo mwaka 1891 katika kijiji cha Qadian kwa makusudi ya kuimarisha imani na kuongeza elimu ya dini na kupata ukaribu na Allah.

Katika mkutano huo, kiongozi wa waaminio huweza kutoa maelezo juu ya maendeleo na changamoto za jamaat Ahmadiyya duniani kote. Wanazuoni pia wa jamaat hupata fursa ya kutoa hotuba za kuimarisha imani za wanajamaat.

Hata hivyo, tukio la kusisimua na kuingeza imani linalosubiriwa kwa hamu na wanajamaat wote ni hilo linaloitwa ***Ba'iat ya Kimataifa.***

Ni katika Baiat hiyo ya kimataifa ndipo nchi ya Tanzania ilipopata baraka ya kuwakilisha bara la Afrika. Itakumbukwa ya kwamba Tanzania ni nchi ambayo imewahi kupata bahati ya kutangazwa na Mwana Aliyeahidiwa, Khalifatul Masih wa II Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad a.s. kwamba ***"Tanganyika ni nchi yetu".*** Ni nchi ambayo pia Khalifatul Masih wa IV Hadhrat Mirza Tahir Ahmad r.h. alipotembelea Tanzania 1988 katika Masjid Salaam alisema ya kwamba ***"kuna mvuto wa ajabu kwenye ardhi ya nchi hii".*** Tuna imani ya kwamba baraka hizi zinatokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Masahaba wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambao walianza kuhubiri ufikaji wa Masihi wakati wa uhai wake.



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a akiongoza Ba'iat ya kimataifa ya mwaka 2018

Ba'iat hiyo ya kimataifa iliyofanyika tarehe 5 mwezi wa nane katika viwanja vya ***Hadeeqatul Mahdi*** huwakilisha wawakilishi wa mabara yote walipo Waahmadiyya ambapo kwa mwaka huu bara letu la Afrika liliwakilishwa na Mjumbe kutoka Tanzania.

Eti Mtume s.a.w Alirogwa? Uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SAMI'INA WA'ATWAANA.

Kijana mbichi, utomvu bado unatiririka usoni. Mafunzo ya dini yake Islam kayaelewa na kuyazingatia vilivyo. Mtu anapotafuta jiko husukumwa na Nasaba, Uzuri, Mali, lakini mwaminio huyaweka kando na ba'id hayo yote na kufuata dini ***RABBANA HABLANA WAMIN AZWAJINA KURRATAN AYYINA.*** Huyo wa kuburudisha macho hapatikani hivihivi kwani *Usione Vyaelea Vyaundwa*. Juhudi zinatakiwa za kulowesha msala kwa dua za vilio. *Wajitahid wajada.*

Sherehe iliyo katika hududi inafanyika. Walima kama desturi siku inayofuata inafanyika. Siku ya tatu inakuja sauti ya Khalifa wa Allah. Hakuna kuongeza neno ila ***Samiina Waatwana***. Wapo kondoo ambao unatakiwa uwaokoe. Kijana anafunga safari kwa miaka kumi na tatu mfululizo. Anapigana jihadi ya mdomo na kalamu. Baada ya miaka hiyo kumi na tatu anarejea nyumbani. Anabisha hodi. Binti anachungulia anamuona mtu ambaye mvi zinaanza kuota. Anakimbia hadi ndani na kumweleza mama yake. *Mama mlangoni kuna mzee*. Mama anajiweka sawa na kwenda mlangoni. Ni furaha na kukumbatiana. Machozi yanatiririka. Binti hajaelewa bado. Mama anamueleza binti *Baba yako huyo*. Binti anamkumbatia huku amefungua mfereji wa machozi. Kama unadhani hii ni hadithi ya kubuni, umekosea sana. Huyo ni mhubiri maarufu wa Islam aliyepigana jihadi. Alipigana jihadi Uarabuni na Ulaya. Mwandishi maarufu wa *Yesu Kafia Wapi*. Aliyepewa lakabu ya ***Khalid*** na Khalifa wa pili Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. Huyo si mwingine bali ni mwanachuoni mahiri Maulana Jalaludin Shams.

Allah Anaeleza kisa cha Nabii Yusuf a.s. katika Quran tukufu na mwisho wa kisa hicho Anasema kuwa *kuna somo ndani yake*. Tunaweza kujifunza mengi katika maisha ya Jalaluddin Shams, lakini somo zito na la msingi ni ***utii kwa Khalifa wa zama***. Hakuna uzima wa kiroho kwa mwaminio bila ya Ukhalifa. Ukhalifa ndio uhai wa Islam. Khalifatul Masih wa I Hadhrat Hakim Nurdin r.a. anasema; mwaminio mbele ya Khalifa anatakiwa awe mithili ya maiti ili Khalifa afanye atakavyo. Uhai wetu. Maendeleo yetu. Uzima wetu, vyote hivyo vinapatikana katika Ukhalifa. Kama asivyoweza kuishi samaki nje ya maji hali kadhalika maji ya mwaminio ni Khilafat na bila Khilafat ni kifo cha kiroho. Ni kifo kibaya kilioje! Allah Atuepushe na hilo.

Ibadhia Kundi la Khawarij

Khawarij ni wingi wa Kharijii. Maana yake ni wajitokezao na washambulizi lakini katika istilahi mradi wake ni watu ambao walijitokeza kutoka jamii ya Islam na walianza kuwashambulia Waislamu. Katika zama za Ukhalifa wa Seyyidna Ali ra. Wakati suluhu ilipatikana kati ya Seyyidna Ali ra. na Amiri Muawia ra. hao jamaa waliinua bendera la uasi na kwa mpango maalumu walijitenga na jamii ya Waislamu na waliendelea kumshambulia Khalifa wa zama na Waislamu.

Na hii pia ni sahihi kwamba katika zama za Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. mbegu ya fitina hiyo ilianza kuota, iliyoimarika katika Ukhalifa wa Seyyidna Ali ra.

Kwa hiyo neno la Khawarij linatumika kwa watu ambao wanaunga mkono itikadi hiyo. Ingawa kwa sababu mbalimbali hao waliitwa pia kwa majina tofauti.

KHARIJII WA KWANZA:

Abdullah bin Nafe Zul-Khawaisara At-Tamimi ndiye mtu awezaye kuitwa Kharijii wa kwanza aliyemtuhumu Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. juu ya ugawanyaji wa dhahabu iliyoletwa kutoka Yemen. Huyo jamaa kwa kiburi sana katika hafla ya halaiki alimsihi Mtume wetu Muhammad s.a.w. kumuogopa Mungu na kushikilia uadilifu. Hapo Mtume Mtukufu s.a.w. alisikitika sana na katabiri kwamba katika kizazi cha huyo jamaa watu watapatikana ambao watasoma Qur'an Tukufu kwa sauti nzuri lakini Qur'an haitateremka kutoka halkumu yao, watajitokeza kutoka dini kama vile mshale unapitia mwili wa mnyama. (Sahihi Bukhari, Kitabul Maghazi Bab bathu Ali bin Abi Talib na Khalid bin Walid kwenye Yemeni. Na. 4351)

Hivi, hao jamaa waliendelea kuzusha fitina katika zama za Mtume Muhammad s.a.w. na Makhalifa wake hata walimwua Hadhrat Uthman ra. Khalifa wa pili. Lakini wakati wa suluhu baina ya Seyyidna Ali ra. na Amiri Muawia ra. hao jamaa walijitokeza na kuasi wazi wazi, walimkufurisha Seyyidna Ali ra. na walipigana naye. Vile vile waliwakufurisha baadhi ya masahaba hata miongoni mwa ***'Ashara Mubashara'*** ambao walibashiriwa Pepo na Mtume Mtukufu s.a.w.

Seyyidna Ali ra. aliwakaribisha katika utii, wengine walimtii Khalifa wa zama na wengine waliendelea kuasi. Kwa mauaji ya masahaba Seyyidna Ali ra. alipigana nao katika vita ya Nahrawan na kuwakimbiza. Abdullah ibn Wahb ar-Rasibi aliwaongoza waasi katika vita. Baada ya miaka mitatu mtu wao Abdur-Rahman ibn Muljam alimwua Khalifa wa Kiislamu Seyyidna Ali ra. kwa jisu wakati alikuwa akisali msikitini.

Kwa viongozi mbalimbali Khawarij waligawanyika



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

katika makundi kwa majina tofauti na waliendelea kuwashambulia Waislamu hapa na pale. Masahaba walikuwa wakiwaita mafasiki kwa sababu ya mwenendo wao. (Sahihi Bukhari, Kitabut Tafsiri, Bab Kul hal nunabbiukum. Na. 4728)

Kwa uasi na ushambulizi wao pole pole makundi yote yaliangamia isipokuwa waliokimbilia na kujificha katika Omani na Yemen.

KUNDI LA IBADHIA:

Khawarij waliojificha na kujisalimisha katika Omani walijiita Ibadhia. Walijiita hivi kwa sababu ya jina la kiongozi wao Abdullah bin Ibadhi At-Tamimi lakini baadhi yao wasema kwamba Jabir bin Abu Zaid ndiye mwanzilishi wao. Bwana Abdullah bin Ibadhi At-Tamimi alizaliwa nchini Omani mwaka wa 18 Hijria na akafia Basra mwaka 93 Hijria. Ukweli ni huu kwamba Bwana Abdullah bin Ibadhi At-Tamimi alikuwa kiongozi wao wa kisiasa na Bwana Jabir bin Abu Zaid alikuwa kiongozi wao wa dini aliyewafundisha mambo ya dini. wote wawili walikuwa katika zama moja. Huyo mzee alifukuzwa huko na Hajjaj bin Yusuf.

Ibadhia wanajipatia majina haya pia: Ahlud-Daawa, Ahlul-Istikama na Jamaatul-Muslimin. Siku hizi Makao Makuu yao ni Oman na wanapatikana katika Algeria, Tunisia, Libya na Zanzibari pia.

ITIKADI ZAO:

*Wanatanguliza kitabu chao cha Hadithi kiitwacho 'Musnad Rabie bin Habib' juu ya Sahihi Bukhari na Sahihi Muslim. Inawezekana sababu ya chuki hiyo iwe Ubainishi wa Unafiki na uasi wao katika Sahihi Bukhari na Sahihi Muslim.

*Wakati wa kuanzisha sala hawainui mikono wala hawafungi mikono katika sala.

*Masuni na Ibadhia wanakatazana kusali nyuma ya wengine.

*Wanayo itikadi kwamba Waislamu wengine minghairi yao wataenda motoni. (Al-Joharul Muktasar uk. 121 na Abu Bakr bin Abdullah Al-Kundi. Lubabul Aathar 1/278 na Mena bin Khalfan) Mungu Atupishe mbali na fitina ya aina aina.

muzaffardurrani@yahoo.com

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Islam na Malezi Bora ya Watoto

Mwl **Issa Salum Disowile**
Shule ya Sekondari Ahmadiyya

Kutoka toleo Lililopita



Mwl **Issa Salum Disowile**
Mwandishi wa Makala hii

HEKIMA

Malezi yetu yanatakiwa yafanyike kwa upole na hekima. Kwani ukali sana hakuibadilishi tabia bali hujenga hofu na uwoga. Qur'an Tukufu inaeleza: "***Uite (watu) kwenye njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako ndiye Humjua sana aliyepotea katika njia Yake, Naye ndiye Awajuaye sana walioongoka***." (An-Nahl: 126)

Hekima uhitaji mwendo wa kiasi. Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema: mwendo wa kiasi ni bora katika mambo yote. Tunapolea tunahitaji kuweka usawa kati ya uzembe na udhalimu **na** uaminifu na mashaka. Vilevile tunapaswa kujua tofauti kati ya kushauri na kuzingatia, ufuatiliaji na kudadisi. Hii ni muhimu hasa watoto wapokuwa katika ujana wao.

Hekima pia inataka tuwajue watoto wetu kwa kujihusisha katika maisha yao kwa mawasiliano ya heshima, kweli na uaminifu. Lazima tujue marafiki zao, maslahi, matarajio, changamoto, mapendeleo, vipaumbele na hali zao. Tunapaswa kuwafundisha, kuwasaidia katika kutatua matatizo yao.

Hata hivyo lazima malezi yetu yazingatie ***islaa***, ambayo ni marekebisho ya tabia. Lazima tutathimini na kufikiria upya juu ya mbinu zetu za malezi, kama matendo yetu na maneno yetu yanapelekea katika wasiwasi na uasi kwa watoto wetu. Tunapaswa kuwa imara lakini wapole kwao.



Kwa upande mwingine, tunapaswa kujua mapungufu yetu na kutafuta msaada wa kitaalamu, ikiwa kuna ulazima, kwa afya ya mwili na akili ya watoto wetu kwa wakati. Udhibiti wa tatizo unaweza kuokoa wengi na kupuuza kunaweza kuangamiza wengi, kwa sababu kuna wakati utalazimika kumwadhibu mtoto ukidhani kwamba hakuelewi kwa kusudi, kumbe ana tatizo ndani ya mwili ambalo linahitaji msaada zaidi.

Hekima pia huhitaji uwezo wa kudhibiti ghadhabu (hasira). Wakati mwingine mzazi anaweza kuwa na hasira ama katibuka, au kachanganyikiwa juu ya mwanawe, au wakati mwingine amechochewa. Baadhi ya hali ni ngumu kujizuia kwa urahisi. Katika kipindi hicho tunahitaji kuonyesha fahari yetu ya malezi



bora, na kujidhibiti na kujiepusha na vitisho visivyo na maana na unyanyasaji wa kimwili au maneno. Yaani tusikimbilie kuwachapa fimbo au kutoa matusi. Masihi Aliyeahidiwa(a.s) alisema:" ***mtu mwenye kujiheshimu na kujidhibiti ambaye pia ni mvumilivu na mwenye heshima, ana haki ya kumrudisha kwa kiwango fulani au kumwongoza mtoto. Lakini mtu mwenye hasira na mkali anayekasirika kwa urahisi hafai kuwa mlezi wa watoto***." (Malfuzat, Jal.2 uk.4).

Kuhusiana na adhabu ya kumchapa mtoto fimbo, Masihi Aliyeahidiwa(a.s) anasema: "***kuwapiga watoto ni kitendo ambacho kinachukuliwa kama ni ushirikina. Pia inamaanisha kwamba mtu mwenye hasira kali hujifanya kuwa ni mshirika wa Allah katika kutoa mwongozo na kuendeleza viumbe.***

Natamani kwamba badala ya kuwaadhibu watoto, wazazi wangeweza kuomba dua, na iwe ndiyo desturi yao ya kuwaombea watoto wao kwa sababu dua ya wazazi kwa watoto wao inakubaliwa na Mungu" (Malfuzat, Jal. 2 uk.4)

KUWA WASTANI

Uislamu unatufundisha kuwatendea watoto wetu kwa wastani na kwa heshima. Mtukufu Mtume(s.a.w) anasema: "***waheshimuni watoto wenu na jengeni tabia njema(nzuri) ndani yao***." (Ibne Majah)

Kila mtoto ana asili na uwezo wa pekee yake, na hata uimara na changamoto zao zinatofatiana. Kwa hiyo kila mtoto anahitaji mbinu zake za malezi. Njia inayomsaidia mtoto huyu haiwezi kumsaidia mtoto mwingine. Hata hivyo, hakuna mtoto anayepaswa kuwa na matatizo yoyote juu yake au ndugu yake kuwa ni mtoto anayependwa.

Hadhrat Nu'man Ibn Bashir(r.a) anasimulia kwamba baba yake alimchukua kwa Mtume Mtukufu(s.a.w) na kusema: nimemzawadia mtoto wangu huyu mtumwa mmoja. Mtume Mtukufu(s.a.w) alimuuliza: umefanya hivyo kwa watoto wako wote? Akajibu: Hapana. Mtume Mtukufu(s.a.w) alisema: zingatia wajibu wako kwa Allah na fanya uadilifu kwa watoto wako. Unataka watoto wako wafanye vivyo hivyo kwako? Akasema: Na'am. Mtume Mtukufu(s.a.w) alisema: Kwa nini sasa na wewe usifanye hivyo kwao? (Bukhari na Muslim, no. 1779 uk.297)

TABIA KWA UJUMLA

Kuhusiana na tabia na mwenendo kwa ujumla, Uislamu unatufundisha: "***Basi shindaneni katika mema.***" (Al-Baqara: 149), hivyo tunahitaji kujenga tamaduni ya kushindana katika tabia na mwenendo na uwezo wa kufanya vizuri katika kila jambo, hasa kwenye kujifunza elimu ya dini na elimu ya kidunia.



Mtume Mtukufu(s.a.w) alisema "***kutafuta elimu ni faradhi kwa kila Muislamu mwanaume na mwanamke.***" (Baihiqi) tunapaswa kujenga tamaduni ya kutafuta elimu na siyo tamaduni ya kutamani fedha. Watoto wetu wasiache malengo yao ya muda mrefu ya kupata elimu na taaluma kwa sababu ya malengo yao ya muda mfupi ya kupata pesa.

Tukiwa kama ni wafuasi na wanyenyekevu wa Mtume Mtukufu(s.a.w) na Masihi wa zama (a.s) sisi na vizazi vyetu tunahitaji viongozi wenye maadili mema na wenye dini wa kidunia, kwahiyo tunatakiwa kuwashinda wengine katika elimu ya kidini na ya kidunia.

WAJIBU WA JAMA'AT

Jama'at ina wajibu gani katika kulea watoto wa Kiahmadiyya? Jambo kubwa ambalo jama'at inalifanya, chini ya nidhamu hii ya Ukhalifa, ni kutualika sisi sote katika kujitolea muda wetu kuitumikia Jama'at. Tunachoweza kukipata kinategemeana sana na jitihada zetu tunazowekeza katika Jama'at. Kama tunahitaji kuwalea watoto wetu vizuri, lazima tuondoe ubinafsi na tuitumikie Jama'at pamoja na familia zetu.

Tushiriki katika shunguli mbali mbali za kijama'at kuanzia ngazi ya familia mpaka taifa, kwa kufanya Wakal Amal, Huduma kwa viumbe, Kueneza Uislamu(Tabligh) n.k

Tuwahimize watoto wetu kujenga tamaduni ya kuangalia ***MTA***, kuandika barua kwa Huzur(a.t.b.a) ili kujenga mahusiano naye, utii kwa Ukhalifa na viongozi wote kwa ujumla, mapenzi ya kusoma vitabu mbalimbali vya Jama'at na hata Gazeti letu hili la ***Mapenzi Ya Mungu.***

Mwisho ifahamike ya kwamba watoto wetu, ni neema na baraka kutoka kwa Allah, na tunapaswa kuwalea kwa upole na uangalifu mkubwa, siku ya mwisho kila mtu ataulizwa juu ya kile alichokichunga. Kuwalea watoto ni jukumu kubwa na gumu kwa kutafuta radhi za Allah. Ikumbukwe Allah anatuonya kwamba: "***Enyi mlioamini, msimfanyie hiana Allah na Mtume hali ya kwamba mnazihini amana zenu mara kwa mara jambo ambalo mnalijua. Na jueni kwamba mali zenu na watoto wenu ni jaribio na ya kwamba kwa Allah yako malipo makuu***." (Al-Anfaal: 28-29)

Malezi yanahitaji subira na sala. Kama tunavyofundishwa kwamba "***ombeni msaada kwa subira na sala***" (Al-Baqara: 154), tunapokwama kimawazo ama kukosa majibu, twatakiwa kurejea kwa Allah kwa kuomba: "***Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu***." (At-Tahriim: 9)

Tunajifunza kutoka kwa Masihi Aliyeahidiwa(a.s) kwa maneno yake kwamba: "***ninawaombea watoto wangu kwa Allah, na kuwaomba wafuate sheria na tabia njema na hakuna zaidi. Zaidi ya hapo ninamtegemea Allah kwa kujiamini kwamba mbegu hii ya bahati iliyopandwa katika kila mmoja wao, itastawi katika muda muafaka***" (Malfuzat, Jal. 2, p.5)

Ninamuomba Allah Atujaalie vizazi vyenye kumuelekea Yeye, na Atuongoze katika kila njia bora ya malezi kwa watoto wetu. Amin.

Wassalaam.

Eti Mtume s.a.w. Alirogwa?

Kuna baadhi ya riwaya zilizoeneza kwa kiasi kikubwa imani za uchawi, Riwaya hizi ni zile zinazoeleza kwamba baada ya mkataba wa suluhu ya Hudaibiyah mtu aitwaye Labid bin Al A'sam alimfanyia ulozi Mtume wetu mtukufu, Muhammad s.a.w..

Inadaiwa ya kwamba mtu huyu aliweka uchawi wake katika kitana au kitu fulani cha kusafishia nywele na kukiweka katika kisima kitumiwacho na Mtume s.a.w..

Riwaya zinadai kuwa Mtume s.a.w. aliathirika kwa uchawi kwa uchawi huo na kubaki akiugua kwa siku kadhaa. Na kwamba miongoni mwa maradhi yaliyomsibu Mtume s.a.w. kutokana na uchawi huo ni pamoja na usahaulifu wa hali ya juu, simanzi na wasiwasi.

Kwa mujibu wa riwaya hizo ni kwamba ilifikia hadi Mtume s.a.w. kusahau kama amekutana na wake zake au la. Inasemwa kwamba Mtume s.a.w. alikithirisha maombi huku akiwa katika mashaka makubwa juu ya hali hii hadi pale Mwenyezi Mungu alipomfahamisha kwa njia ruya kwamba hali hii ilitokana na athari ya uchawi.

Maelezo haya yanapatikana katika kitabu Tabaqaatul kubra cha ibn Sa'd juz. 2, uk 196 – 199 chapa ya Beirut 1957. Pia yamo katika Sahih Bukhari, kitabut tib, babu sihr.

Kwa vyovyote iwavyo, kukubaliana na liwaya hizi kama zilivyo au kwa jinsi zilivyoeleweka na wengi, ni sawa na kuidhalilisha hadhi ya Mtume Mtukufu wa Islam s.a.w.. Daraja lake la kitaqwa, ukaribu wake na Allah na kiwango chake cha juu cha ukweli havitakuwa na maana yoyote iwapo ni kweli kwamba mpuuzi mmoja alifanikiwa kumchezea kwa hila za kichawi na kumwendesha kwa siku kadhaa. Baya zaidi ni kwamba ikiwa kweli Mtume s.a.w. alirogwa, basi ile ahadi ya Mola Wake ya kumlinda dhidi ya watu itathibitika kuwa haikuwa ya kweli.

Mwenyezi Mungu Mtukufu Alimwahidi Mtume wake kuwa atamlinda na watu katika kazi yake ya kueneza ujumbe (Quran Tukufu 5:68), hivyo itakuwa ni jambo la kushangaza ulinzi huu ushindwe kudhibiti hila za mchawi mpuuzi.

Hapa hatumaanishi ya kwamba Mtume wa Allah hakupatwa na maafa yoyote ya kimaumbile. Wao ni wanadamu kama tulivyo sisi, wanakula na kunywa, wanalala na kuamka na bila shaka wanaugua na kufariki. Mtume Mtukufu s.a.w. anaagizwa kupitia Quran Tukufu awatangazie watu kuwa, "***bila shaka mimi ni binadamu kama nyinyi***."(18:111) Kwa hivi hatukanushi kwa Nabii kupatwa na madhara, mashaka na maradhi yaliyo sunna ya kimaimbile kwa mwanadamu. Ila tusichokubaliana nacho ni Mtume Mtukufu wa Allah, Mbora wa viumbe vyote, mwenye ahadi rasmi ya ulinzi wa Mola wake adhurike kwa hila za ubabaishaji wa kichawi.

Manabii wanaweza kudhurika kwa maafa ya kweli tu, kama watanyweshwa sumu, watapigwa mawe, mikuki au mapanga, manaweza kuumia na kudhurika, hii bila shaka ni suna iliyopitiwa na Manabii wote. Lakini uchawi si jambo la kweli katika uwepo wake. Ni uongo uliofurutu ada ambao huwezi kumwathiri mkweli yoyote achilia mbali Mtume Mtukufu, Muhammad s.a.w. aliye mkweli wa wakweli wote, ambaye ujio wake ulikuwa ni kubatilisha uwongo wote kiasi cha kuambiwa useme kuwa; "ukweli umefika, na owongo umetoweka, hakika uwongo ndio wenye kutoweka." (17:82)

Uchawi ni nini?

Katika lugha ya Kiarabu, uchawi huwakilishwa na neno ***SIHR*** ambalo maana yake halisi ni uwongo. Katika kamusi mbalimbali za lugha ya kiarabu maana ya neno hili hufafanuliwa kwa mifano ifuatayo ya matumizi ya lugha; SAHARAHU – KHADA'AHU (amemroga - amemhadaa), SAHARAL FIDH DHAH – TALAAHA BIDH – DHAHAB (ameroga fedha - ameipaka rangi ya dhahabu), AS SIHR; IKHRAAJUL BATIL FII SUURATIL HAQQI (uchawi kuuweka uongo katika sura ya kweli) AS SIHR: MAA YAF ALHUL INSAANU MINAL HIYAL (uchawi lile lifanywalo na mwanadamu kwa hila) ufafanuzi huu umo katika kamusi za Lane, Al Munjid, Lisanul Arab n.k hivyo kimsingi uchawi ni fani ya hila za uongo ambao hauna nguvu yoyote juu ya mtumishi yoyote wa Mungu.



Na **Abdullah H. Mbanga**
99.3 Mtwara

Kwa mujibu wa Qur'an tukufu uchawi ni fani ambayo ilifundishwa na mashetani (2:103). Na bila shaka shetani hana mamlaka na uwezo juu waja wa Allah waliohalisika, kwa hali hii haiwezekani kazi na hila zake zikaweza kumuathiri mja aliyehalisika zaidi mbinguni na ardhini, Hadhrat Muhammad Mustafa s.a.w.

Ndiyo maana dhana ya kuwa Mtume alirogwa inapingwa na maulamaa wakubwa katika Islam.

Mwanazuoni wa kuheshimika mno, Allama ibun qayyim al jawzi anasema; Na kwa wachawi, bila shaka uchawi wao unaweza kuziathiri nyoyo dhaifu na nafsi zenye ufisadi zinazofungamana na upuuzi huo. Huu aghalabu huathiri wanawake, watoto, watu wajinga na wale wasiokuwa na imani thabiti katika dini, wasiotawakali wala kushika tauhidi. (Zadul Maad, juz 5 uk 386)

Mwanazuoni mwingine ni Muhammad Abdul Baqi Zurqani pia ametoa fatwa kama hii alipokuwa akifafanua kauli ya Imam Fakhrud din Razi kwa kusema kuwa; Uchawi hauwezi kudhihirisha athari zake isipokuwa juu ya aliye fasiki. (Sharh mawahib laduniya juz.10, uk. 177)

Hapa inabainika kwamba dhana ya kurogwa kwa Mtume s.a.w ni mtazamo ulio kinyume na mafundisho ya Islam na haiungwi mkono na maulamaa wa Kiislam. Hii ni kutokana na ukweli huu ya kwamba uchawi ambao ni amali ya kishetani katu hauwezi kupenya na kuiathiri dhati tukufu ya Mtume mwenye heshima, Mbora wa Manabii, mtumishi mwaminifu wa Allah, mwenye tabia njema tukufu aliyekuwa saa zote chini ya ulinzi wa Allah.

Mtu mwenye sifa za ukamilifu wa aina hii uliotangazwa na kinywa cha Mungu Mwenyewe, kisha mchawi apate fursa ya kumchezea, siyo tu haiingii akilini, lakini inapingana na uwezo wa Allah, ulio Mkuu na usiomithilika.

MAELEZO YA QURAN TUKUFU

Bila shaka Quran tukufu ilishaeleza kwamba uchawi ni miongoni mwa amali za kishetani, inasema; *Mashetani ndiyo waliokufuru wakiwafundisha watu uchawi*. (2:103).

HIvyo hata kama uchawi ungekuwa nayo athari kweli, bado usingeweza kumuathiri Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. kwa kuwa shetani alishaambiwa na Allah kwamba hatokuwa na mamlaka mbele ya waja wa Allah waliohalisika. (17:66)

Kadhia za matumizi ya uchawi dhidi ya Mitume wa Allah zina historia ndefu, yumkini mashetani wa kila zama walitumia mbinu nyingi chafu kutaka kuwadhibiti Manabii wa zam zao. Uchawi ukiwa ni miongoni mwa hizo, lakini Mwenyezi Mungu alitangaza waziwazi kupitia kitabu chake kitukufu ya kuwa mbele ya Manabii wake; ''wachawi hawatastawi (10:78) na kwamba mchawi hatafaulu popote afikapo (20:70)

Hii inamaanisha ya kuwa hata kuamini kuwa mchawi fulani aliwahi kufaulu kumroga Mtume (s.a.w) ni sawa na kuzikufuru aya hizi za kitabu kitukufu.

Hali kadhalika haya ndio madai ya makafiri wadhalimu dhidi ya Mtume mtukufu (s.a.w) maana ni wao ndio walioeneza uvumi huu kwamba Mtume (s.a.w) ni mtu aliyerogwa. Wanakaririwa na Qur'an tukufu wakiwaambia waaminio ya kuwa; "*ninyi hamfuati isipokuwa mtu aliyerogwa*" (17:48)

Kimsingi dhana hii ya kurogwa kwa Mtume (s.a.w) haiungwi mkono kwa namna yoyote na mafundisho ya Qur'an tukufu. Bali huhesabiwa kuwa ni dhana ya kidhalimu na ni uvukaji wa mipaka dhidi ya heshima ya Mtume (s.a.w)

Hivyo kwa vyovyote iwavyo, dhana hii ni uongo mtupu usio na hata chembe ya ukweli ndani yake. Bila shaka ni uzushi ulioenezwa na maadui wa Islam kwa ajili ya kupandikiza imani zao za kishirikina katika nyoyo za Waislam. Lakini ukweli ni kwamba Mtume mtukufu (s.a.w) hajawahi kuathirika na ulozi wowote katika maisha yake, na kwamba Waislam kamwe hatumfuati mtu aliyerogwa.

NI UPI MSIMAMO WA IMAM BUKHARI

Baadhi ya waumini wa uchawi hutetea dhana yao hii potofu kwa hoja hii kwamba maadam kisa cha kurogwa kwa myume (s.a.w) kimetajwa katika sahih Bukhar, kitabu kiaminikacho zaidi baada ya Qur'an tukufu, basi huenda kuna ukweli juu ya dhana hii.

Ni vyema ikifahamika kuwa Imam Bukhar hakukitaja kisa hiki akiwa kama sehemu ya waumini wa dhan hii ya ulozi.

Iwapo mtu atachunguza kwa makini hekima na mtindo alioutumia Imam Bukhari atagundua kuwa alichofanya Imam Bukhar katika kuijumuisha riwaya hii kwenye sahihi yake ni kukosoa mtazamo huu wa kwamba Mtume (s.a.w) alirogwa. Hii ni kawaida ya uandishi uliotukuka wa Imam Bukhari, kutumia mtindo wa hekima ya kipekee katika kutoa maoni yake juu ya jambo fulani bila ya kutoa maelezo yake binafsi. Ukisoma upangaji wa hadithi, vitabu na milango yake pamoja aya za qurani tukufu anazozitanguliza katika kila sura ya kitabu chake, utabaini kuwa ana maoni gani juu ya riwaya zilizomo katika mlango huo. Na hivi ndivyo alivyofanya katika kitabu chenye riwaya hii ya kurogwa kwa Mtume (s.a.w).

Imam Bukhari ameiweka riwaya hii katika mlango wa tiba (babut tib) akiashiria kuwa maradhi ya Mtume (s.a.w) hayakutokan na kurogwa bali ni ugonjwa wa kawaida ambao ulihitaji tiba.

Aidha aya za Qur'an tukufu alizozinakili na kuzifanya kuwa kichwa cha sura hiyo (kitabut tib) zinaonyesha upinzani wake dhidi ya dhana hii. Miongoni mwa aya alizozinakili ni zilezile zinazopinga nguvu za uchawi dhidi ya watumishi wa Allah. Miongoni mwa aya hizo ni hizi; 2:103, 10:78, 25:9.

Bila shaka Imam Bukhari ametanguliza aya hizi ili kutuzindua kwamba dhana ya kurogwa kwa Mtume (s.a.w) si dhana sahihi kwa mujibu wa Qur'an tukufu hivyo ikiwa msomaji atasoma riwaya hii baada ya kuzitafakari kwa kina na kuzielewa aya zilizotangulizwa na mwandishi katika kichwa cha habari bila shaka atapambanukiwa kuwa uchawi ni uongo wa kishetani tu.

Kwa mtindo wa uandishi wa Imam Bukhari, hadithi zote zilizomo katika kitabu au mlango husika kuwa ni maelezo ya aya anazoziweka katika ufunguzi wa kitabu au mlango huo.

Hali kadhalika Imam Bukhari ameiweka tena riwaya hii katika kitabu *Bad-al Khalq, Babu Siifat Iblis wa Junuuduhu*. Hapa pia alikusudia kuonyesha kwamba ulozi ni miongoni mwa kazi za iblis na kundi lake, na kwa kuwa iblis alishatangazwa kutokuwa na uwezo wowote juu ya watumishi wema wa Allah, basi hila yake yoyote isingeweza kumuathiri Mtume mtukufu (s.a.w)

Mwanazuoni Badrud-din Al-Ain, akisherehesha maelezo ya Sahih Bukhar, anaandika katika kitabu chake *Umdatul Qari* kuwa; "***Imam Bukhar ametaja ulozi na uchawi kwa pamoja kwamba chanzo cha vyote hivi ni shetani, ni kana kwamba hivi viwili ni zao la bonde moja.***" (taz. Babus Sihr)

Bila shaka uchawi ambao ni fani ya shetani hakuna siku uliwahi kumuathiri Nabii wa Allah. Ikiwa kundi kubwa la wachawi wa firauni lilishindwa kumuathiri Nabii wa Allah. Ikiwa kundi kubwa la wachawi wa firauni lilishindwa kumuathiri Nabii wa Israel, Musa (a.s) itawezekanje mchawi mmoja afanikiwe kumuathiri Nabii wa mataifa yote? Kushika dhana hii bila shaka ni dhambi inayohitaji toba ya haraka.

Jamaat Ilivyoingia Katika Kijiji Cha Nyamwilolelwa

Mwl **Ramadhan Mahmood**
Geita

Baada ya watu wa Nungwe kuonyesha msimamo juu ya kuipokea Jamaat sasa hawawezi kuyumbishwa na mtu yeyote. Ndipo nikaona nipeleke ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) katika Kijiji kingine kinachopakana na kijiji cha Nungwe kiitwacho Nyamwilolelwa. Ilikuwa ni tarehe 23/8/2017 nilipokwenda katika katika kijiji cha Nyamwilolelwa kwa ajili ya kuhubiri na siku hiyo nyumba ya kwanza kuingia ilikuwa ni ya bwana Isiyaka Shabani.

Baada ya kuongea nao kuhusu Jamaat, walikubali na nikachukua Baiat zao siku hiyo. Kisha bwana Isiyaka akanipeleka kwa Mzee Masudi Ismail mwenye umri wa miaka 52 na nikaongea nae kuhusu Jamaat, nae hakuwa na kipingamizi basi akajiunga ambae kwa sasa ndie Raisi wa tawi. Watu hao wawili walinipatia ushirikiano mkubwa sana. Kwani nilikuwa natembea nao nyumba kwa nyumba kwa kutumia Baiskeli na idadi iliendelea kuongezeka hadi kufikia 51 waliojiunga na Jamaat ndani ya wiki tatu takribani. Baada ya kufikia idadi hiyo iliyojumuisha wakubwa kwa wadogo, tukaona ni vyema tuanze kusali. Hivyo bwana Ally Charles akajitolea nyumba yake kwa muda ili ibada ifanyike humo. Nyumba ambayo hadi leo tunaendelea kusali ndani yake.


Mwl **Ramadhan Mahmood**
Mkoa wa Geita

UPINZANI ULIJITOKEZA

Katika kijiji hiki pia nilikuta watu wamegawanyika katika makundi matatu, walikuwepo Wakristo na makanisa yao, Wapagani na Waislam wa majina tu kwani elimu ya dini hawakuwa nayo japo walikuwa baadhi ya wakati wakienda kusali Kayenze katika msikiti wa BAKWATA. Lakini leo wote wameipokea Jamaat Ahmadiyya Alhamdulillah. Waislam wa Kisuni wa Kayenze, baada ya kushindwa kuivuruga Jamaat Kijijini Nungwe katika mashauriano yao ndani ya msikiti wao, waliamua kuanza kwenda kijijini Nyamwilolelwa kuwaambia wale waliokuwa wanasali nao kuwa waache Jamaat na kwamba wao kupitia Bakwata Mkoa watawanunulia kiwanja na kuwajengea Msikiti. Lakini wanajamaat kijijini hapa walionyesha msimamo kwa kutowasikiliza wakidai kuwa waliwatelekeza kwa miaka mingi na kwamba wao wameshaipokea Jumuiyya ya Waislam Ahmadiyya. Lakini jamaa hawa wa Bakwata hawakuishia hapo bali walimfuata hata Bwana Ally Charles na kumuomba atufukuze kusali ndani ya nyumba yake, lakini Bwana Ally akawapuuza japo waliendelea kwenda mara kwa mara. Hivyo baada ya kushauriana na viongozi wa kanda, tuliona kuna haja ya kupata mtu wa kuwalea na kuwafundisha watu hawa wa Nyamwilolelwa. Ndipo tarehe 21/11/2017 aliwasili kijijini hapa bwana Abasi Juma kwa ajili ya shughuli hiyo akitokea Bariadi naye anaendelea vizuri kwani mpaka sasa idadi yao imeongezeka hadi kufikia 219. Kwa hakika haya ni matawi ambayo Jamaat inabidi iyatazame sana na kuwapa kipaumbele kutokana na namna walivyoipokea Jamaat na msimamo waliouonyesha dhidi ya upinzani kutoka BAKWATA. Hapa Nyamwilolelwa napo kuna haja kubwa ya kujenga msikiti wa Jamaat kwani idadi yao inazidi kuongezeka.

Karibu Sheikh Musa bin Issa Sahib


Rajabu Abasi Mkieti
Kitonga, DSM

Nifuraha isiyo kifani jumuiya ya waislamu ahmadiyya nchini .Imebarikiwa kupata ujio mkubwa wa Sheikh aliyekua masomoni nchini Ghana. Ikumbukwe kuwa jamaat ahmadiyya duniani ina miliki vyuo vikuu katika nchi mbalimbali ikiwamo Pakistan, Uingereza, Ujerumani, Pamoja na Ghana kwa Afrika. Vyuo hivyo vinatoa toa elimu ya shahada ya juu katika elimu ya dini yaani Shahid. Sheikh Musa sahib alienda nchini Ghana kwa ajili ya masomo ya jamia mwaka 2013 baada ya kuchaguliwa yeye Pamoja na Maulana Sheikh Shabani Shunda kuwakilisha Tanzania katika masomo hayo yalio chukua takribani miaka 5. Mwaka huu 2018 alimaliza jamia na ndipo ilipo takiwa kurudi Tanzania lakini kwa bahati njema Hazrat Khalifatul Masih V atba alitoa agizo kua Wanafunzi wanne walio pata nafasi ya juu katika masomo waende katika mkutano wa mwaka huko uingereza, mmoja wapo katika Wanafunzi walio pata alama zajuu ni Maulana Sheikh Musa sahib. Alhamdulillah Sheikh Musa sahib alijaliwa kuhudhuria jalsa salana yaani mkutano wa mwaka wa uingereza. Ambako huko nako alibahatika kukutana na Khalifa tul masih V ATBA katika ofisi yake na walifanya mazungumzo au Mulaqat katika ofisi ya Khalifatul Masih V a.t.b.a Katika vitu ambavyo Maulana Sheikh Musa alimuomba Huzur nikuombea sana jamaat ya Tanzania pamoja na nchi yetu kwa ujumla. Kwafadhila za Mwenyezi Mungu Maulana Sheikh Musa sahib alijiandaa kurudi Tanzania baada ya mkutano wa mwaka wa uingereza ulio malizika hivi karibuni. Siku ya tarehe 26/08/2018 saa 2 usiku maulana Sheikh Musa aliwasili katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam ambapo alipokelewa na viongozi mbalimbali wa jamaat. Siku ya tarehe 27 ilifanyika tafrija ya kumlaki mida ya saa 8:00 mchana katika ofisi ya Amir jamaat. Viongozi mbalimbali wa jamaat walihudhuria tafrija hiyo. Tafrija ilianza kwa maombi kisha maelezo kwa ufupi juu ya maudhui ya tafrija hiyo yaliyotolewa na Kaimu Amir na Mbashiri Mkuu Maulana Sheikh Abdulrahman M. Ame. Kaimu Amir sahib aliendelea kuelezea kuwa Tanzania imepata baraka kubwa ya kupokea mgeni huyu lakini tuna matarajio makubwa sana kutoka kwa Sheikh wetu kwa sababu amekaa Ghana katika masomo sasa amerudi kuja itumikia jamaat pia na yeye ameipata baraka hii ya kwenda kusoma huko Ghana basi aitumie baraka hii kama kito cha thamani kwa ajili ya maslahi ya jamaat kwa ujumla. Pia nasaha mbalimbali zilitolewa na viongozi kadha ikiwamo Sheikh Bashart sahib, Sheikh Khurram sahib, Sadr Ansarullah na Katibu mkuu wa jamaat ndugu Sefu Hassaan Nakuchima. Katibu mkuu alimuelza Sheikh Musa sahib kuwa jamaat katika nchi yetu imekuwa kwa kasi sana pamoja na kukuwa huko pia changamoto pia zina ongezeka basi ni matarajio ya wana jamaat wa Tanzania yako kwake kwani yeye bado amerudi akiwa ana nguvu kama waswahili wanavyo Sema 'damu changa'. Baadhi ya viongozi walipata kuulizwa maswali kadha juu ya maendeleo ya jamaat ya Ghana. Maulana Sheikh Musa sahib na yeye alipata fursa ya kutoa shukurani zake kwa ukaribisho huo. Baadaye mwisho ilifuata dhifa ya kukata na shoka, kisha kikao kilifungwa kwa maombi yalioongozwa na Maulana Khurram sahib kwa idhini ya Kaimu Amir.


Khalifatul Masih a.t.b.a akiwa katika picha ya pamoja na Sheikh Musa bin Issa baada ya mazungumzo ofisini kwake.

Bustani ya Washairi

WASHAIRI BADO TUPO

Bismillahi naanza, kwako jibu mhariri
Shetani awe wa kwanza, kufukuzwa asikiri
Swali umeliuliza, wako wapi washairi
Washairi bado tupo, Mungu angalituweka

Mungu angali tutunza, mapungufu pate kiri
Binadamu tu wa kwanza, sahau sio kiburi
Sote na tupate waza, watunzi wa mashairi
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Matukio mengi jaza, kwa nini tuwe wasiri
Kweli tuache ajiza, kazi mpe mhariri
Jibule apate jaza, gazetini kuhariri
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Tanga hadi kule Mwanza, tusingoje kukariri
Tungo tupate ijaza, zile zilizo mahiri
Za dini ziwe zaanza, wengi wapate kukiri
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Mirza aliyeanza, dini apate hubiri
Ahmadiyya kuwajaza, kama maji yabahari
Quran waicharaza, kusoma kwa tafakari
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Twaitwa tuwe twajaza, gazetini mashairi
Muhariri aloanza, kutoa ya ubashiri
Hata kule wa Uvinza, tungeniyalo mazuri
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Visiwani muwe kwanza, kumimina misitari
Wa bara tukoe manza, tuungane kwa mahiri
Gazetini kuyapaza, mengi kama utitiri
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Mtwara hadi Uvinza, Kigoma pata habari
Ujumbe huu wafunza, pokeeni kwa uzuri
Malenga mpate kuza, mafunzo ya ushairi
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Dua na iwe ya kwanza, kabura ya kushairi
Mola Apate kuanza, barakaze mtiriri
Ili tupate kufunza, matamu kama sukari
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Hapa natulia kwanza, malenga mtafakari
Musiwe mkajibanza, mjione mafahari
Kazi mpate kwanza, Mungu Atawamahiri
Washairi bado tupo Mungu angalituweka

Hemedi A. Makando
Tanga

WAKANAO MANABII – HAWANAO MWISHO MWEMA

Salam Alaikum, ndugu zangu waadhimu
Ninalo jambo muhimu, hili ninawaletea
Si jipya nawakumbusha, nini Allah Huonesha
Pale watu wakibisha, yale Alowaletea
Mtume anapofika, tusipatwe na wahaka
Na tusiwe na haraka, nje tukamtolea
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Kwanza mpelelezeni, vizuri mchunguzeni
Hata dua pelekeni, kwa Mola wenu Jalia
Muombeni Rahmani, Yeye Awajulisheni
Aliyefika ni nani, na wapi ametokea
Fanyeni hivyo kwa nia, thabiti ya kumjua
Allah Atawaambia, jaribuni mtajua
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Huyo mnayemuhisi, hakutumwa na Kudusi
Kumbe mjumbe halisi, dhambi mtajichumia
Kumkataa hatari, kumkana ni kiburi
Kumkubali kheri, neema nawaambia
Hakanwi yule wa kweli, kumbughudhi muhali
Nawaomba tafadhali, tafakarini jamia
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Ahmadi ni rehema, baraka kubwa kwa umma
Bubu kafanywa kusema, nani asiyetambua
Summu kasikilizishwa, vipofu kawaonyesha
Ni dalili moja tosha, ukweli wa kutujia
Viwete kawainusha, na wagonjwa wa presha
Nyoyo zao kaponyesha, maradhi yamepotea
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Miye nawashaurini, kwa wote wapenda dini
Masihi mumuamini, salama itatokea
Iwapo hatopokewa, watu watambeua
Na kejeli kuitoa, nukusi wajitakia
Huyu Nabii wa Mungu, kumdhihaki ni fungu
Litaloleta machungu, na subhana Jalia
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Kumkashifu Masihi, Masihi wake Ilahi
Haipaswi haisihi, mwatakiwa kuijua
Mtambue hilo kosa, ni kosa kubwa kabisa
Mtajapata mikasa, msiyoitegemea
Nawakanyeni acheni, kiburi ni sheitwani
Na huyo ni maluuni, Mola Amemuapia
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Dhihaka inayotukuka, mnamo hii miaka
Kumtusi na kucheka, ni kutafuta balaa
Balaa mwalitafuta, kwa Yule Alomleta
Allah Atawakamata, kwayo mnayochokoa
Wafasiye mwawaua, mali zao mwachukua
Misikiti mwabomoa, Mungu Awaangalia
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Shufuni ya wale mbele, walifanya mfanyile
Ilifikia kilele, adhabu kuwafikia
Pali na matetemeko, pepo za huku na huko
Kana kwamba ni mahuko mwisho wa hii dunia
Kama hamkubaini, nanyi yatawapateni
Na subiri subirini, Allah Hatowaachia
Masihi ni Ahmadi, Alaihi Ssalaamu
Na yeye ndiye Mahadi, katumwa kwa wanadamu
Kila mja yambidi, akiri amheshimu
Ya Allah ya Maujudi, Mbariki Ahmadi

Al-Ustadhi Mhenga Khamis S.S. Wamwera
0688 -499 996
Kimbangulile – Mbagala Rangi Tatu
Dar es salaam

Mashairi yana utamu wa ajabu. Lakini utamu wa chakula umo katika kukionja na hapo ndipo unapopata elimu yakini. Hatua ya kwanza katika kujenga mahaba na sanaa hii ya ushairi ni kuyasoma. Kuyasoma. Na kuyasoma. Fanya hivi kadri uwezavyo. Tutajitahidi kukuchagulia baadhi ya mashairi yanayokidhi vigezo vya shairi la Kiswahili ili nawe uzame katika ladha hii yenye uwezo wa kukupa maneno mema yaliyoteuliwa vyema. Tunaanza na Mohammed Ali kijana wa Tanga anayetokana na nasaba ya washairi. Itakumbukwa babu yake ndiye aliyeandika Utenzi ule maarufu ***Wajerumani kutamalaki mlima.***

Sanaa ya mashairi, ni sanaa maarufu
Lakini kwa masusuri, ya watu kwa maelfu
Haipati kudhihiri, hata thamani ya dafu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Watu wanashughulika kuyahifadhi magofu
Ipate kusitirika kale ya watu wekefu
Mashairi yakwepeka yasiwe katika safu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Dola ngapi zajipinda sanaa zao kunjufu
Kwa bidii kuzilinda zisipate upujufu
Hawambiwi wanainda shairi wanaposifu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Kama wanavyohifadhi mambo bora manyoofu
Kuitunza yao hadhi wasiwe dola dhaifu
Katu hayawabughudhi mashairi adilifu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Kwani nasi tusihodhi kwa wingi bila ya hofu
Tukaushika waadhi wa wenzetu waongofu
mashairi tukaridhi kuwa ni yetu sharafu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Umondani ya shairi wa taifa utukufu
Kwani zote tafakuri zilo njema na wangafu
Za tangu siku dahari shairini zasadifu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Ushairi ni sanaa tena bora usanifu
Kama vile motokaa wataka utunduifu
Usipoweza zagaa muda si muda ni mfu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Mengi mno kwa machache usemi uso mrefu
Ulojuwa na pekeche zisoleta ukenjefu
Husemeka pasiache hata moja salikifu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Shairi chombo thabiti kipeteshacho marefu
Mawazo mengi ya dhati huyavunga kama ndifu
La kusema silipati johari kuwa zingifu
Wa taifa utukufu umo ndani ya shairi

Mohammed Ali

PANGELIKUWA PAZURI

Pangelikuwa pazuri, tungepata ushahidi
Aliyefunga safari, kuja kwa yake Jasadi
Nasi kutupa habari, aliyoona baidi
Au huku ni kilio, na maradhi yasokwisha?

Mahari penye sururi, palopambwa na waridi
Sehemu ilo na kheri, na wasitani baridi
Pananukia uturi, na thamarati zaidi
Nani aso kimbilia, nieleze nielewe?

Sirudi palipo shari, natamatia na shudi
Sirudi palipo nari, kutesa yangu fuadi
Nimetua niko huri, Namshukuru Wadudi
Hai hata Hai hata, kurudi hiyo safari

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

WAPI ULIPOIONA, BARABARA KUTEMBEA?

Barabara kutembea, jambo kubwa la Ibra
Waitumia jamaa, kuiendesha tijara
Shani kubwa ya Jalia, yatembea barabara
Wapi ulipoiona, barabara kutembea?

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

Hadithi ya Chungu Chenye Ufa

Hapo zamani palikuwa na mtekaji maji huko India aliyekuwa na vyungu viwili vikubwa, kila kimoja kikining'inia kwenye ncha ya mwanzi alioubeba mabegani mwake. Chungu kimoka kilikuwa na ufa ubavuni mwake, na kingine kilikuwa kizima na kikibeba maji kikamilifu mwisho wa safari ndefu toka mtoni hadi nyumbani kwa mwajiri, chungu chenye ufa kikifika na maji nusu tu.

Kwa miaka miwili hili liliendelea, mteka maji akifikisha chungu kimoja na nusu cha maji nyumbani kwa mwajiri. Bila shaka, chungu kizima kilijivunia mafanikio yake, ubora katika kazi yake. Lakini masikini chungu chenye ufa kilijiona dhalili kwa upungufu wake, na uduni wa kukamilisha nusu tu ya ya kazi kilichotengenezewa.

Baada ya miaka miwili ya kujiona mshindwaji mkubwa, kikaongea na mteka maji siku moja mtoni. "Najionea haya, nataka kukuomba msamaha." "Kwa nini?" aliuliza mteka maji?

"Unajionea haya ya nini?"

"Nimekuwa nikifikisha nusu tu ya maji kwa mika miwili iliyopita kwa sababu ya ufa wangu ubavuni mwangu ukisababisha maji kuvuja njiani kote hadi kwa mwajiri wako. Kwa sababu ya upungufu wangu, umekuwa ukifanya kazi kubwa yote hii na kukosa stahiki yako" chungu kilisema. Mteka maji alikionea huruma chungu chenye ufa, na kwa huruma akakiambia, "Tukiwa tunarudi nyumbani, nataka utazame maua mazuri yaliyo pembezoni."

Naam, walipokuwa wakipanda kilimani, chungu chenye ufa kikaona jua likiyaangaza maua mazuri pembezoni, na hili likamfurahisha.



Lakini mwishoni mwa safari, kilijisikia kwa sababu kilivuja nusu ya mzigo wake, na kikaomba msamaha tena kwa mteka maji kwa kufeli.

Mtekaji akakiambia chungu, "Uliona kwamba kulikuwa na maua kwenye upande wako wa njia pekee, lakini si upande wa mwenzako?

Hiyo ni kwa sababu nilikuwa nikiufahamu upungufu wako, na nikautumia. Nimepanda mbegu za maua wa kwako wa njia, na kila siku tukirejea toka mtoni, umekuwa ukiyamwagilia. Kwa miaka miwili nimekuwa nikiyachuma maua haya mazuri na kuipamba meza ya mwajiri wangu. Bila ya wewe kuwa hivyo, asingekuwa na mapambo haya kuipendezesha nyumba yake."

• • • •

Mapitio ya Jalsa Salana Uingereza

Inatoka uk. 1

husababisha kuwataarifu wasiokuwa Waislamu kuhusu mafundisho ya Islam.

Katika hotuba ya siku ya pili ya Jalsa Salana, baraka za Allah zinazopatikana katika mwaka mzima huelezwa kwa kifupi, na twamshukuru Allah kwa sababu ya fadhili Zake zisizohesabika. Sisi tunashuhudia ya kwamba kwa kumshukuru Allah (s.w) baraka Zake zinaanza kumiminika hata katika siku za Jalsa Salana ili tumshukuru zaidi. Na sura yake moja ni maoni ya wageni yahusuyo Jalsa.

Sasa hivi ninapenda kuweka mbele yenu baadhi ya maoni ya wageni, kwayo inadhihirika kwamba baraka za Jalsa zinaleta athari kubwa juu ya wageni.

Mgeni mmoja Bw. Valentine Hudbey aliyetokea nchini Benin alihudhuria Jalsa Salana. Yeye aliwahi kuwa waziri kwa miaka 8 na siku hizi ni mbunge. Amesema katika maoni yake, mimi nimepata katika Jalsa Salana baraka ambazo nisingeweza kuzipata hata kwa kutumia hela nyingi. Nimepata kuishi katika mazingira ya amani na ya kiroho. Mimi sijawahi kuona mkutano wa aina hii wenye nidhamu nzuri ambamo watu takribani elfu arobaini (40,000) walishiriki kutoka mataifa na makabila mbalimbali lakini pamoja na hayo yote utulivu ulipatikana. Hakuna ugomvi wala mapigano. Kila mmoja alikuwa anamhudumia mwenzake. Watoto kwa wakubwa, vijana kwa wazee, kinamama kwa wasichana wote walikuwa wanatoa huduma kwa ajili ya wengine kwa khulka njema. Jambo hili ni lenye kushangaza sana kwamba katika mkusanyiko huu mkubwa wa watu hapana wanajeshi wala polisi, bali wanaoonekana kutekeleza majukumu wote ni wanajumuiya wanaojitolea. Nilikuwa ninafikiria kwamba je, inawezekanaje kufanya kazi za kujitolea bila ya kudai malipo katika zama hizi? Lakini nimefikia hitimisho hili ya kwamba haya yote ni kwa sababu ya uongozi wa Ukhalifa uliowalea watoto, wazee, vijana, na kinamama wa jumuiya kufanya kazi hizo kwa kujitolea. Tangu utotoni huanza kuwapa mafunzo ya kutekeleza majukumu haya. Amesema kwamba Islam inayoelezwa na Jumuiyya ya Waahmadiyya na jinsi Jumuiya inavyotoa malezi kwa sababu, hii hivi karibuni dunia nzima itajiunga na Uislam na Uahmadiyya. Na Uahmadiyya utakuwa dini kubwa kuliko dini zote duniani.

(Kuhusu dini Hudhur alisema) Uahmadiyya sio dini bali dini ni Islam itakayokuwa dini kubwa kuliko zote ambayo ilihuishwa tena kupitia Uahmadiyya na kupitia Seyidna Ahmad (a.s).

(Mgeni) alisema: Mafundisho yanayotolewa na Jumuiya ya Waislamu ya Waahmadiyya ambayo picha yake ya kimatendo inaonekana kwa kushiriki katika Jalsa Salana hii. Mimi ninarudi kutoka London pamoja na kumbukumbu hizi nzuri na bila shaka siwezi kuzieleza ipasavyo.

Kisha mgeni mwingine kutoka nchini Benin Bw. Pascal ambaye ni kiongozi katika wizara ya ardhi, nyumba na maendeleo, amesema: Mimi nimewahi kushiriki katika mikutano mingi, lakini sijawahi kuona nidhamu na mafanikio kama inavyopatikana katika Jalsa Salana yenu. Wafanyakazi katika Jalsa hii walikuwa wanaelewa wajibu wao vizuri na walikuwa wanatekeleza kazi zao kwa namna nzuri. Kuwalisha watu takribani elfu 40, kazi hii ilikuwa si rahisi. Lakini la kushangaza ni kwamba wapishi na wanaopakuwa chakula, wote ni waliojitolea. Ikiwa kazi ifanywe duniani kote kwa namna kama hii, basi mimi ninaamini ya kwamba vita vyote vitaondoka na matatizo yote ya binadamu pia yataondoka. Mimi siwezi kujizuia kusifu Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Kila mwanajumuiya akiwa kijana, mtoto, msichana, kinamama hawa wote wana nidhamu nzuri na utaratibu mzuri.

Mwakilishi wa Rais wa nchi ya Haiti Bw. Joseph alishiriki Jalsa na akasema: Uzoefu huu wa Jalsa Salana ni uzoefu mzuri sana ambao siwezi kuusahau. Mwenendo usio na mfano wa wafanyakazi umeniathiri sana hata kuyabadilisha kabisa maoni yangu yahusuyo Uislamu.

Kutoka Ivory Coast Jaji wa Mahakama kuu Bw. Tube Ally pia alihudhuria Jalsa salana. Yeye pia ni mshauri wa tume ya katiba ya kitaifa ya Ivory Coast. Amesema: Mimi mwenyewe ni Muislamu na tangu miaka 20 niliwahi kushiriki katika mikutano ya kidini ya madhehebu mbalimbali ya Waislamu. Lakini katika miaka hii 20, mimi sikupata elimu ile ya Uislamu ambayo nimeweza kuipata katika siku hizi tatu za Jalsa salana. Maendeleo ya kiroho niliyopata katika siku hizi tatu sikuyapata katika miaka 20 iliyopita. Maulamaa ambao si wanajumuiyya wao hawana kitu chochote, ikiwa mtu anataka kujua kuhusu mafundisho sahihi ya Kiislam basi yeye ajiunge na Jumuiya. Kisha amesema: Jinsi wafanyakazi walivyokuwa wakijitolea katika Jalsa, inathibitika kwamba Wanajumuiya wanapenda sana Ukhalifa na kwa sababu ya upendo huu humtii Khalifa wao na kuishi kwa udugu. Umoja unapatikana katika upendo huu. Ndio maana wanaweza kutoa huduma sahihi ya Uislamu. Dhehebu lolote jingine la Waislam halina kiongozi kama huyu wala umoja kama huu. Amesema nitahudhuria Jalsa Salana katika siku za usoni na nitamleta mke wangu pia.

Kisha kutoka Belize mwandishi wa habari amesema: Mimi nilipopanda ndege kutoka Miami kwenda London nilikuwa na hofu kubwa na mawazo mbalimbali ya kutisha kichwani mwangu. Mawazo haya hayakuwa kwa mujibu wa urefu wa safari ya masaa 7, bali nilikuwa na hofu na wasiwasi ya kwamba siku 3 zajazo nitashinda pamoja na Waislamu. Baadhi ya Waislamu huhusika na matukio ya ugaidi yanayopatikana duniani. Nilifikiria ya kwamba ndege imekwisharuka kwa hiyo mimi siwezi kurudi na sasa lazima nikabili hali hiyo ngumu. Mimi nikafanya dua ya kwamba nisisibiwe na shambulio la ugaidi. Kama hali ilivyo, sijasibiwa na shambulio lolote bali kweli ni kinyume chake kabisa. Mimi nilikalishwa hapa kama Malkia na athari niliyopata katika Jalsa Salana ni ya aina ya kipekee katika maisha yangu. Nilikutana na watu wengi katika maisha yangu lakini ni kweli, sijawahi kuwakuta watu wenye huruma kama wanajumuiya. Mimi nilikuta Jumuiya yenye uzuri wa hali ya juu. Nilipata kuona viwango vya hali ya juu vya upendo na unyenyekevu. Kila siku ilikuwa ya ajabu mno. Mimi nina fahari kwamba ninarudi baada ya kujenga urafiki na marafiki wengi na pamoja na kumbukumbu nzuri. Kwa kweli uzoefu huu ulikuwa wa aina ambayo sitaweza kuusahau katika maisha yangu.

Kisha Meya wa mji wa Belize Bw. Bernard Joseph amesema: Uzoefu wangu wa kwanza wa Jalsa Salana ulikuwa mzuri wenye kuridhisha sana. Siku zote tatu nimevutiwa sana na udugu wa wanajumuiya, upendo kati yao na huduma zao kwa wanadamu. Mimi nimetokea nchini ambamo tunakabili matatizo mengi ya kijamii. Mimi kwa kuwa Meya wa Belize naona kwamba kwa ajili ya kuondolea mbali matatizo haya huenda tupate mwongozo kutoka Jumuiya ya Ahmadiyya huko Belize. Amesema mimi ninarudi pamoja na kumbukumbu nzuri na mahusiano tuliyoyajenga katika siku hizi tatu. Huduma za malazi, chakula na usafiri zilipangwa vizuri sana. Madereva wa magari, wafanyakazi waliokuwa wanawakaribisha wageni kwenye kiwanja cha ndege, katika Jalsa watoto waliokuwa wanatakeleza jukumu la kugawa maji, wale wanaosimimia maegesho ya magari, vile vile wale waliokuwa wanapika chakula na uongozi wote uliokuwa unapata kuhudumu bila ya kuonekana, wote walishirikiana kuifanya Jalsa hii iwe yenye kukumbukwa daima.

Kisha kutoka Italia Profesa mmoja alikuja aitwaye Bw. Nastola Kosvalibalda. Yeye ni Padre katika Kanisa la Roman Katoliki na aliwahi kuwa mshauri wa Papa wa zamani. Amesema: katika Jalsa Salana mimi nimekuta hasa mambo haya matatu; la kwanza ni kukutana kwa watu wa mataifa mbalimbali na upendo mkubwa bila ya kuwa na chuki yoyote, bila shaka ni jambo la ajabu mno. Hatuwezi kupata hali kama hii katika dunia nzima. Jambo la pili ni utulivu nilioupata katika Jalsa Salana na hakuna jambo lolote la kutia wasiwasi; na jambo la tatu ni kwamba hotuba za Khalifa zilikuwa na ujumbe uliobainika na ndani ya hotuba zake zimo nasaha nzuri zinazoweza kutekelezeka.

Kisha kutoka Ufilipino mgeni mmoja alikuja aitwaye Belina Rubus anayefanya kazi katika *Arab News*, mwaka jana alihudhuria Jalsa Salana kwa kuwa Mwandishi wa habari wa gazeti lake na mwaka huu pia ameshiriki kwa kutumia nauli yake. Yeye amesema katika maoni yake: Mwaka huu nimekuja mara ya pili kuhudhuria Jalsa Salana, ninalazimika kusema haya ya kwamba kila mara nimevutiwa sana na mipango na nidhamu ya Jalsa Salana. Vile vile kwa kuona hali ya kiroho ya Wanajumuiya na hususan jambo hili ya kwamba watu wa mataifa mbalimbali wamekuja katika Jalsa Salana kwa ushirikiano mzuri na tofauti ya taifa lolote au rangi yoyote huwa haionekani. Huu ndio udugu na upendo unaowezesha mafundisho yenu yafuatwe. Mwenendo huu una athari zaidi idumuyo kuliko hotuba zote. Mimi nina yakini kwamba washiriki wote hurudi na mazingira ya upendo na usawa katika nchi zao na hivyo nchi zote zinazoshiriki katika Jalsa, huweza kunufaika na mazingira haya. Amesema sawa na mtazamo wangu watu wengi wanatakiwa kuishi kwa siku kadhaa pamoja na wanajumuiya katika mazingira ya Jalsa ili wao pia waweze kujua kwamba upendo na udugu ni nini na picha halisi ya Uislamu ni nzuri kiasi gani.



Khuddam Washiriki Ijtimaa Kenya



Mnamo tarehe 08.08.2018 ujumbe wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ulielekea jijini Nairobi nchini Kenya kuhudhuria na kushiriki Ijtemaa ya Kenya. Ujumbe ulijumuisha ndugu wanne yaani Abdallah Msesemele, Jalaluddin Mbawala, Juma Mpondo na Yuusuf Mgeleka kisha jioni hiyo waliwasili ndugu wanne kutoka Uganda na usiku majira ya saa nane aliwasili Sadr sahib wa Nigeria. Siku ya Alhamisi tulikuwa na mwenyeji wetu Sheikh Abdullahi Juma aliyetutembeza markaz yote na kutuonyesha shughuli mbalimbali zinazofanyika pale ikiwemo Kiwanda chao cha uchapaji na namna ambavyo hufanya Jalsa Salana zao.

Siku ya jumamosi ilisheheni mashindano kuanzia asubuhi mpaka usiku ambapo sisi tulishiriki mpira wa wavu, kupimana misuli, ta'alim, chemsha bongo na mpira wa miguu bila kuambulia ushindi. Ujumbe wa MKA Tanzania ulishiriki pia mashindano ya kiujumla ya utoaji khutba (speech) na mshindi alikuwa ni ndugu Yuusuf Mgeleka kutoka Tanzania, mashindano ya ushairi mshindi alikuwa ndugu Jalaluddin Mbawala toka Tanzania. Washindi wote walitunukiwa nishani siku ya kilele cha ufungaji wa Ijtemaa, Alhamdulillah.

Siku ya kilele ilifana sana kwa ushiriki mzuri, ukumbi kupendeza na matayatisho yavutiayo. Kaimu Amir Jamaat Kenya alikuwa mgeni rasmi katika uhitimishaji kwa hotuba yenye nasaha.

Ujumbe wa Tanzania ulipata nafasi pia ya kuhitimisha ufungaji huo wa Ijtemaa kwa desturi yetu ya kughani shairi la " kwa heri ya kuonana" lenye kawaida ya kuwadondosha machozi ndugu washiriki na kuziamsha hisia kiasi cha ukumbi mzima kusimama na kupunga mikono ya "kwaheri". Tuliondoka nchini Kenya tarehe 14.08.2018

Ukweli wa Seyidna Ahmad a.s.

Kabla ya kuingia katika mada nimeonelea nieleze japo kwa ufupi Seyidna Ahmad a.s. ni nani? na ukweli wake ninaotaka kuuthibitisha ni upi?.

Seydna Ahmad a.s. alizaliwa mwaka 1835(1250H.J.) katika kijiji cha Qadiani katika jimbo la Panjab nchini India. Mwaka 1882 alijitangaza kuwa Allah Amemteua kuwa Mtume Wake katika zama hizi. Alitangaza kuwa Allah Amempatia cheo cha Umasihi katika zama hizi na Mahdi.

Kutokana na madai hayo niliyoyataja hapo juu katika zama hizi.Kama ilivyo ada kwa wanadamu kila wafikiwapo na ujumbe wa kiroho basi huzalika makundi mawili:

Kundi moja wanayaamini hayo madai yote ni ya kweli na yametoka kwa Allah kupitia kwa Seydina Ahmad (a.s.) moja kwa moja bila shaka yoyote.

Na kundi la pili linakataa katakata na linasema aliyedai madai hayo ni muongo na hakutumwa na Allah (Mungu Apishe mbali). Kwa hiyo makala haya ni yakuwathibitishia kundi la pili Seyidna Ahmad (a.s.) ni mkweli katika madai yake yote. Hivyo naomba msomaji wa makala haya fuatana nami neno kwa neno katika kuthibitisha ukweli wa Seyidna Ahmad (a.s.). Ili kuelewa ukweli wa Mtume au Nabii yeyote ni lazima tupate mizani ya kupimia kwa neno zima swali hili lazima lijibiwe, je Mitume na Manabii hutambuliwaje?? Jibu la swali hili Allah Amelijibu kwa uwazi kabisa katika Quran tukufu pale aliposema: "*Na tuliviangamiza vizazi vingi kabla yenu pindi walipodhulumu, hali ya kwamba Mitume waliwafikia kabla ya hapo, wakiwa na Ishara waziwazi lakini hawakuwa wenye kuamini. Hivi ndivyo Tuwalipavyo watu wakosefu*." 10:14.

Allah Akasema tena.

..."*Na haiyumkiniki Mtume kuleta Ishara isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila muda unayo hukumu*." 13:39

Seyidna Ahmad (a.s.) naye kwa kujibu swali hili alisema:

"*Ni jambo la kawaida kwamba njia ya kuwatambua Manabii na Mitume wa Mwenyezi Mungu ni miujiza na ishara zao. Kama mtu akipewa na serikali mamlaka, hupewa alama fulani, vivyo hivyo kwa kuwatambua Mitume wa Mwenyezi Mungu pia kuna ishara. Nami nasisitiza kusema kwamba Mwenyezi Mungu kwa kunisaidia Amedhihirisha ishara, si moja, si mbili wala si mia mbili bali malaki, na hizo si ishara ambazo hakuna asiyezijua, bali malaki ya watu wamezishuhudia.*

Nami naweza kusema kwamba hata katika mkutano huu pia mamia ya waliozishuhudia wanaweza kuwepo. Ishara zimedhihirika kwa ajili yangu toka mbinguni na ardhini pia. Ishara zilizohusika na madai yangu ambazo zilitabiriwa mapema na Manabii wengine na Mtume saw, pia zimetimia."(Hotuba ya Ludhiana Uk.50)

Kwa neno zima tunaelewa kwa uwazi ukweli wa Mtume au Nabii yeyote anajulikana kwa ishara zake alizopewa na Allah kwa hiyo ni rahisi kumjua mwongo na mkweli kwa kutumia kipimo cha ishara. Kipimo hiki (ishara) ndicho Allah alichokisisitiza mara kwa mara kila Mtume au Nabii alipewa ishara zake ambazo zikitizamwa kwa uaminifu ukweli wake utadhihirika. Na wenye nia safi na walio waaminifu katika nyoyo zao watamkubali kwa urahisi. Na kipimo hiki (ishara) hakuna mwanadamu anayeweza kujivisha bali Allah ndiye anayewavisha watumishi wake waliotakasika kabisa (Mitume). Kama Allah alivyobanisha: "*...Na haiyumkiniki Mtume kuleta Ishara isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila muda unao hukumu*". (13:39)

Pia Allah Amewawekea Manabii au Mitume uadui katika ishara zao ili kupitia uadui wa ishara zao watu walio na nyoyo za uaminifu ambao wanatafuta ukweli wataweza kudhihirikiwa ukweli kwa urahisi zaidi. Kama Allah alivyobainisha.

"*Na kama hivyo tukamfanyia kila Nabii adui, mashetani katika watu na majinni. Baadhi yao wanawafunulia wengine maneno ya ushaufu kuwadanganya*" (6:113)

Pia Allah Akaendelea kubainisha tabia za maadui wa Mitume na Manabii kwa kusema.

. "*Na hakuwafikia Mtume yeyote isipokuwa walimfanyia mzaha*." (15:12)

. "*Na hakuwafikia Nabii yeyote ila walikuwa wakimfanyia mzaha*." (43:8), "*Na wanapoiona Ishara hufanya mzaha*." (37:15)

Kutokana na tabia hizo za uadui Mitume hupata wakati mgumu sana katika kazi zao kiasi kwamba ukweli wao huanza kutiliwa shaka kwa sababu mara nyingi maadui wa Mitume huwa wengi, wenye nguvu, wenye mali, wenye mamlaka ya kiutawala n.k.w. Kama Allah alivyobainisha:

"*Na Hatukumtuma Mwonyaji kwenye mji wowote ila matajiri wa mji ule walisema, Kwa yakini sisi tunayakataa hayo mliyotumwa kuyaleta." "Na wakasema: Sisi tunazo mali nyingi na watoto wengi, wala sisi hatutaadhibiwa.*" (34:35-36.)

"*Na kadhalika Hatukumpeleka Mwonyaji katika mji wowote ila matajiri wake walisema: Kwa yakini tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na hakika sisi tunafuata nyayo zao. Akasema: Hata kama nawaleteeni (desturi) yenye mwongozo bora kuliko mliyowakuta nayo baba zenu? Wakasema: Kwa hakika sisi tunayakataa yale mliyotumwa nayo. Ndipo Tukawapatiliza, basi angalia ulikuwaje mwisho wa wale waliokataa Mitume*."(43:24-26.)

"*Basi walipowafikia Mitume wao kwa dalili zilizo wazi wakafurahia elimu waliyokuwa nayo, na yakawazunguka waliyoyafanyia mzaha*." (40:84)

"*Na kadhalika Tuliwaachia viongozi wa wakosefu katika kila mji wafanye hila humo dhidi ya haki; wala hawafanyii hila isipokuwa nafsi zao, lakini hawatambui*." (6:124)

"*Na inapowafikia Ishara, husema: Hatuwezi kuamini mpaka tupewe sawa na yale waliyopewa Mitume wa Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye Ajuaye zaidi Atakapoweka ujumbe Wake. Hivi karibuni itawafikia fedheha kutoka kwa Mwenyezi Mungu na adhabu kali kwa sababu ya hila walizokuwa wakifanya*."(6:125)

Aya hizo zimetuweka wazi daima maadui wa Manabii/ Mitume wanakuwa ni watu wenye heshima zote katika jamii zao yaani mali, elimu na utawala kwa hiyo wanapoamua kukataa jambo wanakuwa na uwezo wote wa kibinadamu wakulizuia na kulifuta kabisa.

Kutokana na nguvu waliyonayo maadui wa Manabii hakuna akili ya mwanadamu inayoweza kuwaza namna maadui wa Manabii wanaweza kushindwa katika mapambano yao. Ni desturi iliyowazi kabisa serikali yenye nguvu kubwa ya kiuchumi na majeshi yaliyo imara ndio yenye uwezo wa kushinda kila aina ya vita. Na haitegemewi wala haidhaniwi nchi yenye uchumi dhaifu na majeshi dhaifu iingie katika vita na nchi yenye uchumi mkubwa na majeshi imara kisha nchi dhaifu ndio ishinde vita dhidi ya nchi iliyo imara. Hivyo basi inapotokea mtu dhaifu kumshinda mtu aliyeimarika. Ni lazima kila mtu atajuwa kwa uwazi zilikuwepo sababu zisizoonekana kwa macho zilizosababisha ushindi huo. Na hivyo ndivyo ilivyo daima Mitume huwa wanasaidiwa na Allah kwa hiyo anayepingana na Mitume hiyo anapingana na Allah. Kwa hiyo haiwezekani Allah Ashindwe katika mapigano yoyote. Maana yeye mwenyewe amejiwekea ahadi hii.

"*Mwenyezi Mungu Amekwishaandika bila shaka Nitashinda Mimi na Mitume Wangu! Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye heshima*." 58:22

"*Bila shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi,*"40:52

Kwa hiyo kupitia ushindi waupatao Manabii/ Mitume basi huwa ni dalili tosha ya ukweli wao. Na kupitia uadui ukweli wa Mitume hudumu katika zama zote katika hali iliyokuwa wazi kama jua na Allah Akatujengea msingi huu:

"*basi angalia ulikuwaje mwisho wa wale waliokataa Mitume*."(43:26)

Hivyo kila ichunguzwapo historia ya maadui wa Manabii/Mitume basi ukweli hujidhihirisha kama mwanga wa jua na kupitia hapo hakuna mtu yeyote mwenye moyo wa uaminifu anayeweza kupinga hivyo kila atafutaye ukweli basi hubainikiwa ukweli wa Nabii wa zama zake.

Hivyo tuchunguzapo historia ya Firauni tunadhihirikiwa ukweli wa Nabii Musa (a.s.) kwa uwazi usiobakisha shaka yoyote kwa kila mtu aliye mwanifu wa moyo.

Halikadhalika tuchunguzapo historia ya Abuu Lahabi na Abuu Jahali pamoja na maadui wengine wengi wa Mtume (s.a.w) tunadhihirikiwa na ukweli usioweza kupingwa na mtu yeyote mwenye moyo wa uaminifu. Hivyo hivyo kama tutakavyokuja kuona kutoka kwa Seyidna Ahmad (a.s.) ndani ya upinzani alioupata kuna ishara nyingi zenye kuthibitisha ukweli wake. Hapo nimejaribu kueleza kwa ujumla namna Mitume walivyoweza kupata uadui na ndani ya uadui kulikuwa na ishara nyingi na mpaka sasa hakuna mtu yeyote mwaminifu anayeweza kusema kughalikishwa kwa firauni hakukuwa ni ishara.



Ahmad Abdul Bishazo
Kiwalani, Dar es salaam

Na wala hakuna anayeweza kusema maswahaba 313 (r.a.) wenye silaha dhaifu wasiokuwa na uzoefu wa vita walioshinda katika vita (Badr) dhidi ya jeshi la watu 1000 wenye silaha imara na wazoefu wa vita sio ishara. Au kifo cha Abuu Jahal na Abuu Lahabi sio ishara. Halkadhalika kwa Manabii wengine zipo ishara nyingi za namna hiyo. Hivyo kutokana na makala haya yanakusudia kueleza ukweli wa Seyidna Ahmad (a.s.) katika madai yake ya utume, sina budi kueleza ishara zake ambazo ndani mwake wapinzani waliomuita muongo Allah aliwaadhibu kwa adhabu iliyodhihilika kwa uwazi ni ishara ya kuthibitisha ukweli wake na hivyo ndivyo ilivyokua kwa Manabii wa kabla yake. Nitaanza kwa kueleza ishara moja Seyidna Ahmad (a.s.) ambayo ilitabiriwa karne nyingi kabla ya kuzaliwa kwake ambayo ishara hiyo inahusu adhabu kwa wale watakaompinga na kumfanyia uadui Seyidna Ahmad (a.s.). Nayo ndio hii:

"*Na Hatukumtuma Nabii yeyote katika mji wowote isipokuwa Tuliwashika wenyeji wake kwa taabu na mashaka ili wapate kunyenyekea*."(7:95)

Mambo mawili yanaonekana katika Aya hii: (1) Misiba yenye kuenea kote-kote haiwafikii watu mpaka Nabii wa Mungu ametumwa;

(2) ni jambo lisilotokea kuwa kufika kwa Nabii wa Mungu kusifuatane na misiba iliyozagaa. Jambo ambalo ni la lazima Nabii yeyote lazima apingwe akiwa mkweli atapingwa na akiwa muongo atapingwa. Akiwa muongo watakaompinga watakua ndio wakweli. Na hatimaye nabii wa uongo hatafaulu maana Allah Atawasaidia wakweli na hiyo ni sunna Yake. Ama akiwa ni Nabii mkweli watakaompinga ndio watakua waongo na Allah lazima Awaadhibu waongo na adhabu hiyo itakuwa ni ishara isiyoweza kupingika wala kutiliwa shaka yeyote. Kama Allah Alivyobainisha.

"*Ndipo Tukawapelekea tufani na nzige na chawa na vyura na damu kuwa Ishara zielezazo; lakini wakatakabari na walikuwa watu wakosefu. Na ilipowaangukia adhabu, wakasema: Ewe Musa, tuombee kwa Mola wako yale Aliyokuahidi; kama ukituondolea adhabu, bila shaka tutakuamini na kwa yakini tutawapeleka wana wa Israeli pamoja nawe*." 7:134-135.

Pia Mtukufu Mtume (s.a.w) alipata kuomba adhabu ili iwe msaada wa kukubaliwa ukweli wake.

Imam Bukhari anasimulia ya kwamba "Makureishi walipozidi kumpinga Mtume (s.a.w.) aliomba waadhibiwe kwa njaa kama iliyotokea siku za Nabii Yusuf. Basi Makureishi walipata njaa kali kwa miaka saba hata wakawa wanakula mifupa na mizoga, nao walipokuwa wakitazama mbinguni walikuwa wanaona kama moshi kwa ajili ya shida."

Hakika ishara zenye adhabu huwa hazibakishi shaka yoyote ndio maana firauni pamoja na kibri chake baada ya kuiona adhabu alikili Nabii Musa (a.s.) ni mkweli na mungu wake ni wa ukweli. Hivyo basi tutaiona miji ilioangamia na kupata misiba mingi ya kila aina ambazo ni ishara za ukweli wa Seyidna Ahmad (a.s.). Katika mwaka 1882 Seyidna Ahmad (a.s.) alipata ufunuo kutoka kwa Allah (s.w.) uliokua ukimtambulisha ni Mtume wa Allah. Ufunuo huo ni mrefu ninanukuu baadhi ya maneno kutoka katika ufunuo huo.

"*Ewe Ahmad! Mwenyezi Mungu Ameweka baraka ndani mwako, sio wewe uliyetupa kile ulichotupa, bali ni Allah Ndiye Aliyetupa. Mwenyezi Mungu Amekufundisha Kurani, yaani Amekudhihirishia maana zake zilizo sahihi, ili uwaonye wale watu ambao mababu zao hawakuonywa, ili ibainike njia ya wakosefu, kwamba ni nani anayetengana nawe. Sema mimi nimetumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na mimi ni wa kwanza wa wenye kuamini. Sema: Haki imekuja na batili imekimbia na batili huwa ndio yenye kukimbia. Kila baraka imetoka kwa Muhammad s.a.w. Hivyo amebarikiwa sana yule aliyetoa elimu na yule aliyepokea elimu. Na watasema kwamba huu sio Wahyi Bali ni maneno tu aliyoyabuni mwenyewe. Waambie kuwa ni Allah Aliyeyateremsha maneno haya, kisha waache wachezecheze ndani ya mawazo yao potofu. Waambie: Kama maneno haya ni uzushi wangu na sio maneno ya Mwenyezi Mungu basi mimi ninakuwa ni mwenye kustahili adhabu kubwa sana....*" (TADHKIRAH.Uk.56-HAQIIQATUL WAHYI)

Baada ya Seyidna Ahmad as kupata ufunuo huu alianza kupata upinzani na uadui mkubwa kutoka kila upande viongozi wa dini zote wakaungana katika kumfanyia kila aina ya uadui. Na hapo ndipo zile adhabu zilizokuwa zimetabiliwa kabla ya kuzaliwa kwake zikiwa ndizo ishara zake zilizosema hivi.

"*Na hukumu itakapotolewa dhidi yao Tutawatolea kiumbe kutoka ardhini ambacho kitawajeruhi kwa sababu watu hawakuziamini Ishara Zetu*." (27:83)

Sawa na aya hiyo hapo juu khalifa wa pili r.a. alisema hivi. "*Kudhihiri kwa tauni kulitabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. katika njia mbili. Pengine aliueleza kama Daabba (mdudu) wa ardhi. Maelezo haya ni kweli kwa sababu tauni inaletwa na kuumwa na kiroboto. Hiki kiroboto hutoka chini na kuuma mwili wa mwanadamu. Quran Tukufu imetumia jina hilihili. Huu siyo ugonjwa wa kawaida. Ni ugonjwa wa dunia ambao umeleta vifo na maangamizi sehemu nyingi sana*."(Wito kwa Mfalme Muislam uk.105)

Halikadhalika Mtume (s.a.w) aliendelea kutoa bishara ya ugonjwa wa tauni katika fafanuzi mbalimbali.

..."*Hapo Nabii wa Allah, Masihi na maswahaba wake wataelekea kwa Allah na watamuomba Allah Awatumie maadui mdudu wa ugonjwa wa tauni,...*" (Muslim. No. «1808»)

Pia Mtume (s.a.w) aliendelea kufafanua.

Anas r.a. amesimulia ya kuwa "*atakapotokea Dajjal na keelekea Madina, ugonjwa wa tauni utatokea duniani*." (Kwa upokezi wa Tirmidh, Hadith no. «2408»)

Mtume (s.a.w) aliendelea kutoa tabiri juu ya ugonjwa wa tauni (daabba=mdudu) pamoja na ishara zingine.

Alisema kwamba: "*Kiama haitatokea mpaka mmone kabla yake ishara kumi. Moshi, Dajjali, Mdudu, uchomozi wa jua kutoka magharibi, ujio wa Isa mwana wa Mariamu, Yajuji na Majuji, kupatwa kwa mwezi mara tatu, Kupatwa katika mashariki na kupatwa katika magharibi na kupatwa katika bara Arabu na ishara ya mwisho ni Moto utokao Yemen utakaowapeleka watu kwenye mwisho wao.*"

(Sahihi Muslim, Kitabul Fitan, bab Ashratus Saa?) (Hadith. «7467»)

Itaendelea toleo Lijalo

MATUKIO KATIKA PICHA



Khalifa mtukufu akisalimiana na Amir jamaat Tanzania alipotembelewa ofisini kwake hivi karibuni



Khalifatul Masih akiongoza Du'a katika moja vikao vya Jamaat nchini Uingereza



Sadr Ansarullah Bw. Ali Khamis Mbambwa sahib akiwa na baadhi ya wajumbe wa tanzim kwenye banda la Tabligh mjini Bukoba



Baadhi ya wajumbe wa tanzim ya Ansarullah wakiwa na Mbashiri wa mkoa wa Dodoma Sheikh Khawaja Muzaffar



Jamaat Ahmadiyya kanda ya kusini walipokuwa na kikombe cha ushindi baada ya kushika nafasi ya tatu kwenye maonyesho ya Nanenane 2018



Kaimu Amir Kenya pamoja na Khuddam wa Kenya na Tanzania nje ya Msikiti wa Nairobi



Lajna Imaillah Tanzania wakiwa katika Waqar-e-mal ya maandalizi ya Jalsa Salana ya 2018



Kikombe walichoshinda Ahmadiyya cha mshindi wa tatu taasisi za kielimu kwenye maonyesho ya Nanenane



Mtoto ambaye hakupatikana jna lake kwa haraka anayekadiriwa kuwa na umri chini ya miak 2 akiiangalia kwa umakini mkubwa picha ya Khalifa wa zama



Khalifa mtukufu akiwa na Atfal na Nasrat wa Kenya alipotembelea Kenya 2005

Watu Walio Bora Kabisa

Inatoka uk 12

tena na aliyetabiriwa kuja atakuja chini yake hiyo ndiyo tunayoijua kupitia hadithi za mtume saw na kupitia Qurani Tukufu.

Mtume saw alimuungaisha hadhrat Aamir na hadhrat Yazid bin Munzir katika udugu wa Muakhaat. Hadhrat Aamir bin Rabia alifariki siku chache baada ya kufariki kwa hadhrat Othman r.a.

Swahaba wa pili ni hadhrat Haram bin Milhan. Hadhrat Haram Bin Milhan alitokana na ukoo wa Ansar uitwao bani Adi bin Najjar. Jina la baba yake Milhan alikuwa Malik bin Khalid. Jina la mama yake Haram bin Milhan lilikuwa Malika binte Malik. Dada yake alikuwa Umme Sulaim ambaye alikuwa mke wa hadhrat Abu Talha Ansari ra na mama ya hadhrat Anas bin Malik. Dada yake wa pili hadhrat Umme Haram alikuwa mke wa hadhrat Ubada bin Samit. Hadhrat Haram bin Milhan alikuwa mjomba wa Hadhrat Anas. Alishiriki katika vita vya Badri na Uhud na aliuawa kuwa Shahidi siku ya Be'are Mauna.

Anas bin Malik anasimulia kuwa watu kadhaa wakaja kwa mtume saw. na kumwomba kwamba; Uwatume pamoja nasi watu ambao watufundishe Qurani na sunna, naye alituma pamoja nao maswahaba 70 wa Kiansar, waliokuwa mahafidhu wa Qurani na mjomba wangu Haram pia alikuwa miongoni mwao. Watu hawa walikuwa wanasoma Qurani na wakati wa usiku kulikuwa na darasa la kujifunza elimu, na mchana kuleta maji na kutunza msikitini na kukusanya kuni huko porini na kununua nafaka kwa kuiuza kwa ajili ya watu wa Suffa na mafukara.

Nimeshaeleza kidogo juu ya hadhrat Haram bin Milhan katika hutuba yangu ya Ijumaa niliyoitoa miezi kadhaa iliyopita wakati wa kueleza tukio la Be'are Mauna na katika maeneo mengine pia, sasa ningependa kuweka mbele yenu baadhi ya riwaya za Bukhari ambayo hayajaelezwa hapo awali.

Imesimuliwa na hadhrat Anas bin Malik kwamba, hadhrat Haram bin Milhan alipopigwa mishale ya siku ya Be'are Mauna basi akachukua damu yake na kupaka kwenye uso na mikono yake na kusema fuztu bi Rabbil Kaabah, yaani naapa kwa Mola wa Kaaba kuwa nimeshapata kusudio langu.

Imesimuliwa na hadhrat Anas ra kwamba watu wa makabila ya Re'l, Zakwan, Usayya na banu Lahyan wakaja kwa mtume saw na kusema tumeshasilimu na kumwomba mtume saw msaada juu ya watu wao na mtume saw aliwasaidia kwa watu 70 Maansar. Hadhrat Anas alikuwa anasema kwamba sisi tulikuwa tunawaita maqaari, hawa walikuwa wanakusanya kuni mchana kutwa na kusali usiku mzima. Wale watu wakawachukua na wakati walipofika kwenye Be'are Maun basi waliwadanganya na kuwaua na mtume saw aliomba dua kwenye sala juu ya kabila la Re'l, Zakwan na banu Lahyan kwa muda wa mwezi mmoja au kwa siku 40 sawa na riwaya zingine.

Imesimuliwa na hadhrat Anas kuwa Mahuffaz hawa walipouawa basi mtume saw aliomba dua kwa uyenyekevu kwa muda wa mwezi mzima na riwaya nyingine ya Bukhari iko hivi kwamba mimi sijamwona mtume s.a.w. kuhuzunika zaidi ya tukio hilo.

Kisha kuna riwaya hii pia kutoka kwa hadhrat Anas kwamba mtume saw aliendelea kuomba dua akiwa amesimama baada ya rukuu, juu ya baadhi ya makabila ya banu Sulaim. Yeye alisema mtume saw aliwatuma maqari 70 kwa watu washirikina ambao wakawazuia (kwenye sehemu yenye kisima iitwayo Maun) na kuwaua ilhali kulikuwa na mkataba baina yao na baina ya mtume saw. Kisha riwaya nyingine pia inasema kuwa sijamuona mtume saw akihuzunika kwa yeyote mwingine jinsi alivyohuzunika kwa mahuffaz hawa.

Kisha kuna hawala ya sirate ibne Hilbiyya kwamba Jabbar bin Salma alikuwa na Jabbar bin Tufail, wakati ule na kusilimu baadaye, anasema sababu ya kusilimu kwangu ni hii kwamba nilipiga mishale baina ya mabega ya mtu mmoja nami niliona kwamba mishale ilipita kwenye kifua chake kisha nilimsikia yule mtu akisema fuztu wa Rabbil Kaabah yaani naapa kwa Mola wa Kaaba kuwa nimeshapata kusudio langu, ndipo nilijiuliza amefuzu vipi huyu je sijamuua huyu? Jabbar anasema niliuliza baadaye juu ya kauli yake hii na watu walijibu kwamba maana yake ni kupata daraja la Ushahidi. Jabbar anasema nilinena kwamba amefaulu kwa kweli mbele ya Mungu. Maneno ya aina hii yamesimuliwa na watu wawili au watatu wengine pia. Hawa ni watu ambao kusudio lao hasa lilikuwa kupata radhi ya Mwenyezi Mungu na mafanikio ya dunia hayakuwa shabaha yao, kisha Mwenyezi Mungu pia alisema kuwahusu wao kwamba Yeye amewaridhia kutokana na nia yao ya aina hii. Maswahaba waliomba dua hii wakati wa kuuawa katika Be'are Mauna ... kwamba Ewe Mwenyezi Mungu umjulishe mtume saw juu ya hali zetu kuwa sisi tumeshakutana na Wewe na Wewe umeturidhia nasi pia tumeridhika kwako. Hadhrat Anas anasimulia kwamba Jibraeil a.s. akaja kwa mtume saw na kumpa habari hii kuwa maswhaba wake wale wameshakutana na Mwenyezi Mungu na Mungu amewaridhia.

Hadhrat Mirza Bashir Ahmad ra. anaeleza kuyahusu matukio ya Be'are Mauna na Raji'i kuwa kutokana na matukio haya inaeleweka husuda na bughudha kubwa kabisa ya makabila ya Waarabu waliyokuwa nayo vifuani mwao juu ya Islam na Waislamu hata walikuwa hawaoni aibu katika kusema uwongo na udanganyifu mkubwa na waislamu pamoja na kuwa hodari na wenye akili walikuwa wanadangnyika kutokana na busara na dhana nzuri ya uaminifu wao. Mahuffaz, wenye kusali sala za kawaida hata za tahajjud na wenye kukaa msikitini na kumkumbuka Mungu kisha maskini waliokuwa wanashinda na njaa ambao waliitwa na hawa wadhalimu kwenye nchi yao kwa nia ya kujifunza dini na walipofika kwao kama wageni wao waliwaua bila kuwahurumia. Mtume saw. hata kama angehuzunika zaidi kutokana na matukio haya isingetosha, lakini yeye hakuchukua hatua yoyote ya kivita dhidi ya wadhalimu hawa, alihuzunika lakina hakupigana vita juu yao, ila kuanzia siku ile ya kupata habari zao hadi siku 30, kwenye kila sala yake ya asubuhi aliomba dua dhidi ya makabila yao ya Re'l, Zakwan, Usayya na banu Lihyan kwa uyenyekevu mkubwa mno, na kumuomba Mungu kwamba Ewe Mola wangu, uturehemu juu ya hali zetu na kuyazuia mikono ya maadui wa Islam ambao wanaendelea bila huruma kumwaga damu za Waislamu wasio na hatia, ili wafute dini yako.

Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. akasema na hata leo hii pia maombi yanahitajika kwa ajili ya kuyazuia mikono ya maadui wa dini na kupata msaada wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Afanye mpango wa kuwashika na kutufanyia urahisi na wepesi.

Kulikuwa na swahaba mmoja Hadhrat Sa'ad bin Khaulah r.a. ambaye sawa na baadhi ya simulizi yeye alikuwa mtumwa aliyepata uhuru kumpitia ibn Abi Ruham bin Abdul Uzzah Aamri. Yeye alisilimu na anahesabiwa miongoni mwa Sabeqiin (waliotangulia kuamini, waliosilimu mwanzoni mwa Uislam) alikuwa miongoni mwa waliohamia Uhabeshi mara ya pili. Hadhrat Saad bin Khaula alipohama Makka na kuhamia Madina basi alikaa kwa Hadhrat Kulthum bin Hazm. Ibne Is'hak na wengine walimuhesabu miongoni mwa watu wa Badri.

Hadhrat Saad bin Khaula aliposhiriki katika vita vya Badri alikuwa na umri wa miaka 25. Yeye alishiriki katika vita vya Uhud na Khandaki na mapatano ya Hudaibiyya. Hadhrat Saad ra alikuwa mume wa hadhrat Subaya Aslamiya ra. Yeye alifarika wakati wa Hijja tul Wida'a na mtoto wake alizaliwa baada ya muda mfupi ya kufariki kwake na mtume saw alimuambia mke wake kwamba sasa baada ya kuzaliwa kwa mtoto huyu unaweza kufunga ndoa na yeyote utakayempenda. Hakuna aliye na wazo tofauti juu ya wakati wa kufariki kwake katika Hijja tul Wida'a isipokuwa Tabri na kwa mtazamo wake yeye alifariki kabla ya Hijja tul Wida'a.

Kisha kuna swahaba mwengine Hadhrat Abul-Haitham Malik bin Tayyihan Ansari ra. Jina lake sahihi lilikuwa ni Malik, lakini anajulika kwa jina lake maarufu la lakabu Abul-Haitham. Mama yake Laila binti A'tiiq alitokana na kabila la Bali. Wahadithina wengi wanasema ya kwamba Bali ni tawi moja la kabila la Aus. Hadhrat Abul-Haitham alikuwa anachukia kufanya ibada ya masanamu hata kabla ya ujio wa Islam na alikuwa ana mtazamo wa umoja wa Mungu tangu utoto wake. Muislamu mmoja alipohama kutoka Makka na kuhamia Madina na kueneza habari za Uislamu, Hadhrat Abul-Haitham ambaye muda wote alikuwa akitafuta ukweli mara moja akampokea na kukubali dini tukufu ya kiislamu basi akahamia Makka na kujiunga na uislamu.

Hadhrat Mirza Bashir Ahmad RA akimtaja katika kitabu chake cha Sirat Khatamunabiyyin anasema ya kwamba huyu alikutana na Mtume s.a.w.katika bonde fulani na kumpa habari za Madina na baiat yake ilikuwa msingi imara wa dini tukufu ya Islamu katika Madina. Baiat (kiapo chake cha utii) kilikuwa hivi: Sisi Tunamuamini Mungu Mmoja, Hatutamshirikisha na chochote, hatutafanya zinaa, hatutafanya mauaji, hatutamsingizia mtu yeyote na tutakutii katika kila kitendo chema.

Baada ya kuchukua baiat hii mtume Muhammadi (s.a.w) alisema kama mtashika ahadi hii kwa uimara mtaingia peponi lakini mkionyesha udhaifu bila shaka Mwenyezi Mungu ndie atakaye watendea apendavyo.

Baiat hii aliyoichukua kwa mkono wa mtume Muhammad (s.a.w) huitwa Bait-e-'Aqbah Ula (yaani Baiat ya kwanza ya 'Aqabah. 'Aqbah ambayo maana yake ni njia ya mlimani iliyoinuka ni sehemu iliyopo baina ya Makka na Minaa. Sahaba huyu alikuwa miongoni mwa watu sita wa kabila lake waliokwenda Makka kwa ajili ya kufanya baiat na kurudi Madina na kuueneza ujumbe wa Islam.

Kuna simulizi inayosema kwamba yeye ndie mtu wa kwanza kutoka Madina aliyekwenda Makka kufanya baiat kwa mkono wa mtume Muhammad (s.a.w) na wahadithina wanakubaliana ya kwamba katika wakati wa Bait-e-'Aqbah Thania (yaani Baiat ya Pili 'Aqbah) mtume Muhammad (s.a.w) alipopanga viongozi kumi na mbili na yeye alikuwa pia kati ya viongozi hawa.

Kuna hadidhi nyingine ambayo inasema kwamba safari moja hadhrat Abul-Haitham alisema ewe mjumbe wa Allah (s.a.w) sisi tuna mikataba mingine na makabila mengine sasa sisi tutakapoingia katika Islam utakapotuamuru kutenda kuhusiana na mikataba hii ndivyo tutakavyotenda lakini ningependa nikuombe ya kwamba sasa tumeungana na wewe na Mwenyezi Mungu atakapokusaidia na kukujaalia ushindi basi nakuomba usituache na kuirudia kaumu yako. Hapo mtume s.w.a akatabasamu na kusema damu yako ni damu yangu, mimi natokana nawe na atakayepigana nawe atapigana nami na atakae kuwa radhi nawe basi nami nitakuwa radhi naye.

Inasimuliwa ya kwamba safari moja Hadhrat Abul-Haitham alimuandalia chakula mtume (s.a.w) na maswahaba zake; Mtume (s.a.w) alipomaliza kula akawaambia maswahaba ya kwamba wampe malipo yake Hadhrat Abul-Haitham. Hapo maswahaba wakauliza tumpe malipo gani ewe mjumbe wa Allah. Mtume (s.a.w) akasema mmoja wenu anapofika kwenye nyumba ya mwenzake na kunywa maji au kula chakula inabidi amfanyie maombi ya kwamba Mwenyezi Mungu amlipe malipo mema.

TANGAZO LA JALSA SALANA TANZANIA 2018

Amir na Mbashiri Mkuu nchini anapenda kuwaarifu Wanajumuiya wote kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 28, 29 na 30 Septemba 2018, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah. Hivyo tunatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Wanajumuiya wote wajitahidi kuhudhuria Jalsa hiyo na ihakikishwe kwamba kusiwepo hata tawi moja katika kila mkoa ambalo halitokuwa na angalau mtu mmoja atakayehudhuria Jalsa.

2. Masheikh na walimu wajitahidi sana kuwakumbusha wanajuiya juu ya umuhimu na baraka za kushiriki kwenye Jalsa Salana kwa nauli zao wenyewe. Pia kwa vile wanajumuiya wa mkoa wa Dar es Salaam kimsingi hawahitaji nauli ikilinganishwa na wale wa mikoani basi wote wasikose kuhudhuria Jalsa hiyo.

3. Marais wa mikoa na viongozi wengine wa Majlis za matawi nao wajitahidi kuhudhuria Jalsa Salana kwa nauli zao.

JALSA SALANA TANZANIA MUBARAK

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

DH. QAD - DH. HIJ 1439 AH | SEPTEMBA 2018 | IKHA 1397 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Said Khudri r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Jihadi bora ndiyo kusema neno la adili mbele ya Sultani mdhalimu. (*Tirmidhi*)

Watu Walio Bora Kabisa

Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Leo nitaeleza tena habari za masahaba kadhaa waliojaaliwa kushiriki katika vita vya Badri, Hadhrat Aamir Bin Rabiyya ra ndiye sahaba wa kwanza nitakayemtaja.Ukoo wake ulikuwa na urafiki na baba yake Hadhrat Umar (r.a) aitwaye Khattab, aliyemfanya Hadhrat Aamir kuwa mwanawe, ndiyo sababu mwanzoni alikuwa anajulikana kwa jina la Aamir bin Khattab lakini amri ilipotolewa na Kurani Tukufu ya kuwa kila mmoja anasibishwe na wazazi wake wa kweli basi badala ya kuitwa Aamir bin Khattab kutokana na jina la baba yake Rabiyya akaanza kuitwa Aamir bin Rabiyya. Huzur akasema: "Hapo jambo limekuwa wazi kwa wale wanaowalea watoto wa jamaa zao na watoto hao wanakuwa hawajui kwamba wazazi wao wa kweli ni kina nani? Na katika vitambulisho vyao na kwenye nyaraka za serikali badala ya kuandika jina la baba zao wa kweli jina la yule anayekuwa amewalea huandikwa kisha kutokana na hilo matatizo mbali mbali huzalika. Kisha watu wananiandikia barua ya kwamba kifanyike hiki na kile, hivyo siku zote yatupasa tutende sawa na maamrisho ya Kurani Tukufu. Labda ukiwaacha watoto wale wanaotolewa na idara fulani na taarifa za wazazi wao hazitolewi.

Kwa vyovyote baada ya ufafanuzi huo ninaeleza machache kuhusu sahaba huyo. Kama ilivyokuwa imeelezwa kuwa kulikuwa na urafiki kati ya makabila yao, Hadhrat Umar ra na Hadhrat Aamir walibaki kuwa marafiki mpaka kifo chao na Hadhrat Aamir ra alijiunga na Uislamu katika siku za mwanzo na alipojiunga na Uislamu Mtume saw alikuwa bado hajaingia kwenye Dar e Arkam.

Hadhrat Aamir ra alihamia Uhabeshi kisha akarudi Makka, tena akahamia Madina pamoja na mke wake Laila Bint Hathmah. Yeye alikuwa mwanamke wa kwanza aliyehamia Madina. Hadhrat Aamir ra alishiriki vita vya Badri na vita zingine pamoja na Mtume saw na alifariki dunia katika mwaka thelathini na mbili wa kihijiria.

Hadhrat Aamir ra anasimulia ya kwamba, Mtume saw alimwambia: "Mmoja wenu akiliona jeneza na asiwe na nia ya kushiriki katika jeneza hilo basi inabidi asimame mpaka jeneza lile limpite au liwekwe chini." Hadhrat Abdullah bin Aamir ra anasimulia kutoka kwa baba yake Hadhrat Aamir ra ya kwamba: "Usiku mmoja aliposimama kwa ajili ya sala, huu ulikuwa ni wakati ambapo watu walikuwa wanafanya maongezi yasiyofaa dhidi ya Hadhrat Othman ra yaani ulikuwa ni mwanzo wa fitina katika Islam na walikuwa wanatumia lugha chafu dhidi ya Hadhrat Othman ra. Yeye anasema kuwa baada ya sala alipopata usingizi akaona kwenye ndoto ya kwamba aliamrishwa asimame na amwombe Mwenyezi Mungu ili Mwenyezi Mungu Amwepushe na fitina hii ambayo Huwaepusha nayo waja Wake walio wema, hivyo Hadhrat Aamir ra aliinuka na akasali na kumwomba Allah juu ya hilo, hivyo baadaye akaumwa na hakutoka nyumbani kwake mpaka kifo chake, kwa uchache Mwenyezi Mungu Akamsaidia kuepukana na fitina hii kwa namna hiyo.

Hadhrat Aamir ra anasimulia ya kwamba: "Mimi wakati wa kufanya Tawwaaf nilikuwa pamoja na Mtume saw, ndipo kamba ya viatu vya Mtume saw ilikatika nikamwambia Ewe Mtume wa Allah, nipatie niitengeneze, Mtume saw akasema, hapana hii ni kama kujipendelea nami sipendi nipendelewe. Kwa kiasi hiki Mtume Mtukufu saw alikuwa makini katika kufanya shughuli zake mwenyewe.

Mtu mmoja alimjia Hadhrat Aamir bin Rabiyya ra akiwa mgeni wake naye akamhudumia vizuri na kumheshimu mno na akaeleza mambo yake kwa Mtume saw. Mgeni huyo alitoka kwa Mtume saw na kuja kwake na kusema: "Nilikuwa nimemwomba Mtume saw bonde fulani ambalo mfano wake haupatikani katika Uarabuni mzima nalo Mtume saw amenipatia tayari sasa napenda nikupe sehemu yake moja ambayo iwe ya kwako katika maisha yako na baada yako vizazi vyako viwe vinairithi, Hadhrat Aamir ra akamjibu kuwa, mimi sina haja yoyote ya kupata sehemu yake kwani leo sura fulani imeteremka iliyotufanya tuisahau dunia nayo ni hii: Imewakaribia watu hesabu yao nao wamo katika mghafala wakikengeuka. Hii ilikuwa hali ya Nyota hawa waliokuwa wakin'gaa kwa kumwogopa Mwenyezi Mungu na kuwa na hofu Yake na kwa kweli hao ndio walikuwa wenye kutanguliza dini juu ya dunia.

Hadhrat Aamir bin Rabiyya ra anasimulia ya kwamba Zaid bin Ammr alisema, "mimi niliipinga kaumu yangu na kufuata mila ya Ibrahimu. Mimi nilikuwa namsubiri nabii mmoja ajitokeze kutoka kizazi cha Nabii Ismaili ambaye atakuwa anaitwa Ahmad lakini najihisi ya kuwa sitaweza kumpata yeye, hivyo mimi namwamini na kumsadikisha, ninatoa shahada kwamba yeye ni nabii ikiwa mtabahatika kupata zama zake basi mumfikishie salamu yangu. Mimi nawaambieni alama zake zitakazodhihirika juu yenu. Yeye siye mrefu mno au mfupi sana, nywele zake zitakuwa za wastani, muda wote macho yake yatabaki kuwa mekundu, muhuri wa utume utakuwa kati kati ya mabega yake, jina lake litakuwa Ahamd, mji huu wa Makka utakuwa mahala pa kuzaliwa kwake kisha watu wake watamfukuza humo na watauchukia ujumbe wake kisha atahamia Yathrab kisha atapata ushindi, nyinyi msije mkajidanganya. Mimi nikitafuta suna ya Ibrahimu nimejihangaisha sana, nimewauliza Mayahudi, Wakristo na wanaoabudu moto nao wakasema kuwa dini hii ndiyo itakayowafuata nyinyi. Nao wakaniambia alama zile zile nilizozieleza kwenu, nao wakasema kuwa hakuna mtume yeyote ajaye baada yake, Hadhrat Aamir ra alisema, "Mtume Mtukufu saw alipodhihiri nilimweleza habari hizi za Zaid, Mtume saw alisema, "nimemwona huyu peponi alikuwa anajisogeza mbele."

Kuna riwaya kuwa, hatakuja nabii, si maana yake kwamba bishara ile iliyotolewa na mtume saw kuhusu ujio wa umaati nabi sio sahihi bali maana yake ni hii kwamba atakayekuja (atakuwa mfuasi wake) na yeye ni mwisho wa kuleta sheria na hakuna sheria itakayokuja

Endelea uk. 11

Umrah (Hija Ndogo) - Sehemu ya Pili

Na **Ali R. Mohammed - Safarini Qatar**

Wakati tumemaliza Yale ya Muhimu katika kukamilisha Ibada ya Umrah ndani ya Masjid Haraam, kabla hatujaingia sehemu inayofuata. Tuangazie maeneo muhimu yanayozunguka Masjid Haraam ambayo yana umuhimu wa kipekee kwa kuwa yanagusa historia ya dini yetu tukufu ya Islam.

MAENEO YA KIHISTORIA KATIKA MASJID HARAAM

Kwa kawaida, baada ya kumaliza ibada hii Haji ndogo yaani Umrah, iwapo hujaji bado ana siku za kutosha Makkah, anaweza kuendelea kuhudhuria sala za faradhi masjid Haraam, pamoja na sala, pia hujaji anaweza kuendelea kuizunguka Kaaba huku akiendelea kumtukuza Allah Mtukufu, mizunguko 7 akiwa na mavazi yake ya kawaida, wakati wowote kabla na hata baada ya sala za faradhi, kama ni nyakati za mchana hata Usiku.

Hujaji ataendelea kumtukuza zaidi Allah pamoja kusoma Quran tukufu na kufanya toba na Istighfar na maombi, kwa maana hii ndiyo nafasi pekee ya kuonyesha ukaribu kwa Mola wako.

Baada ya kumaliza siku 3 kati ya sita za uwepo wangu Makkah, shauku yangu ilikuwa ni kutaka kujua masuala kadhaa pamoja na kuyaona kwa macho yangu ambayo tulijifunza huko nyuma kupitia vitabu na vyuo vyetu katika jamaat juu ya Islam na historia yake. Kwa bahati nzuri nilitumia muda mwingi kuuliza maswali kadhaa kwa ndugu mmoja toka Sudan tuliyekuwa naye katika msafara ule ambaye amekwisha fanya Umrah mara nane (8).

Tukianza na mwonekano wa Masjid Haraam wa sasa ni tofauti na miaka ya nyuma. Wakati huo mji wa Makkah ulikuwa mdogo, na hata idadi ya Waislam ilikuwa ndogo wakati ule wa Mtume s.a.w hasa baada ushindi wa Makkah.

Bonde la Masjid Haraam lilikuwa na makazi na nyumba yaliyokaribiana sana eneo la Kaaba. Hivyo kutokana na ongezeko la waumini waliofika toka sehemu mbalimbali kwa ajili ya ibada za Haji na Umrah, eneo la msikiti mtukufu liliendelea kupanuliwa miaka yote kuendana na ongezeko la watu. Hivyo hata makazi yaliyokaribia sana yalilazimika kuondolewa ili kupisha upanuzi huo wa Masjid Haraam.

Hivyo katika harakati za upanuzi wa Eneo la Masjid Haraam, yako maeneo Ambayo yalikuwa muhimu sana yakibeba matukio makubwa katika historia ya Islam, ambayo yalilazimika kuondolewa ili kupisha upanuzi wa msikiti, na hata yale ambayo yamesalia, hayajaandikwa wala kuwekwa alama zozote. Mmoja kati ya wale nilikuwa nawauliza maswali mbalimbali, aliniambia kuwa watu tunatofautiana mioyo na imani zetu. Wako ambao walizitumia alama hizo vibaya kwa kufanyishwa hata yale ambayo Mtume s.a.w aliyakataza. Wengine walifanya ibada na kusali na kusujudu mbele ya vitu ambavyo haikupaswa kufanywa hivyo. Ilizuka mikusanyiko ya aina mbalimbali hata sehemu hazikupaswa kufanywa hayo hasa Yale yaliyoashiria ushirikina bayana.

Ili kudhibiti haya, mamlaka husika walilazimika kuondoa baadhi ya alama katika maeneo muhimu, na hata yale yaliyobaki hayajawekwa alama au utambulisho wowote.

Mfano mmoja mdogo tu ambayo ulinistua nilipopewa habari zake, ni juu ya ***Makkah tower*** au ***Masjid Haraam tower*** (ambayo nitaielezea baadae) kuwa eneo lile ambapo inasemwa kulikuwa na shina au kisiki cha mtende ambacho Mtume s.a.w alitumia kama mimbali kuegemea wakati akihutubia, kuwa shina au kisiki kile kiliisha kwa kumegulimeguliwa vipande na waumini na kuondoka navyo, ambao walifika pale kwa ajili ya ibada huku wengine wakisujudu na kusali pale.



Picha ya zamani ya Kaaba wakati makazi ya wenyeji yalipokuwa yakiizunguka, ambapo kwa sasa eneo hilo lote liko ndani ya Masjid Haraam.

Itaendelea toleo lijalo